# MAADILI YA MT. FRANSISKO WA ASIZI

## MAZINGIRA YAKE

Asizi ni mji wa Italia, mkoa wa Umbria, wilaya ya Perugia. Ndiko alikozaliwa mtakatifu Fransisko. Wakati wake kulikuwa na mageuzi makubwa katika jamii na hata vita vingi. Vilianzishwa viwanda vingi vidogovidogo ambavyo viliwavuta wengi wakimbie mashamba na kuhamia mijini; biashara ilizidi, hivyo wakaanza kupatikana watu tajiri sana, mmojawao baba yake, Petro wa Bernardone.

## MATUKIO YA MAISHA YAKE

1181 Mtoto Yohane alizaliwa na kubatizwa. Baba yake akirudi toka safarini akamtajia jina la Fransisko, yaani Mfaransa Mdogo. Baada ya hapo mtoto akalelewa katika anasa, ingawa hatujui kama ujanani aliulinda usafi wa moyo au sivyo. Kwa tabia alikuwa na uchangamfu na huruma sana kwa maskini ila aliogopa wenye ukoma. Pamoja na adabu njema alipewa pia elimu kidogo kupitia mapadri, halafu akawahi kuanza biashara.

1198 Huko Asizi vilianza vita vya wenyewe kwa wenyewe: inawezekana Fransisko naye alishiriki kushambulia na kubomoa ngome ya kifalme iliyokuwepo juu ya mji huo.

1202 Asizi ulishindwa vitani na jeshi la Perugia; Fransisko mwenyewe akatekwa na kufungwa huko Perugia. Wakati huo wa mateso alianza kukomaa na kubadilika kimawazo. Baada ya mwaka mmoja akarudishwa nyumbani kwa sababu ya ugonjwa na kisha kulipiwa pesa nyingi ili aachiliwe.

1204 Fransisko aliendelea kuugua mwaka mzima.

1205 Fransisko aliondoka tena aende vitani kujipatia sifa na cheo katika kuikomboa nchi takatifu ya Yesu, lakini kabla hajatoka mkoa wake akarudi Asizi kutokana na njozi na sauti aliyoisikia. Akaenda Roma kuhiji kwenye makaburi ya Mitume, alipobadilishana nguo na fukara na kuanza kuombaomba. Katikati ya mwaka uongofu wake ulikuwa umekomaa: katika karamu ya mwisho aliyowaandalia wenzake alikuwa akifikiria kuoa bibi ufukara. Alipokutana ghafla na mkoma akashuka kwenye farasi akamsaidia pesa akambusu: ndio ushindi mkuu uliofanya kuanzia hapo kusiwe na kitu cha kumzuia. Karibu na mwisho wa mwaka akamsikia Yesu msalabani akimuambia, "Fransisko, nenda ukarekebishe Kanisa langu, kwa kuwa linataka kubomoka": ndiyo kazi ya utawa atakaoanzisha, ingawa mwanzoni alielewa tofauti, kwamba arekebishe magofu ya kanisa aliposikia sauti hiyo.

1206 Baada ya miezi ya mashindano na wazazi wake, waliokuwa wakimshutumu na mara kumbembeleza mara kumtesa, mwanzoni mwa mwaka Fransisko aliitwa hukumuni kwa meya. Lakini kama mtu wa Mungu akakataa mahakama ya serikali, hivyo kesi ikafanyika mbele ya askofu Guido. Hapo alimkataa baba yake pamoja na mali za urithi hata akamrudishia nguo zake zote. Baada ya kuishi kidogo kama boi kwa Wabenedikto, akahamia Gubbio alipovaa kanzu ya mkaapweke, akawa anasali na kutumikia wakoma. Mnamo Julai akarudi Asizi arekebishe kanisa la mtakatifu Damiano ambapo alitabiri watakuja kukaa masista watakatifu.

1207 Alirekebisha kanisa la mtakatifu Petro na mwisho lile la mtakatifu Maria wa Malaika: kazi za ukarabati zilichukua karibu miaka miwili, kwa kuwa mwenyewe alikuwa akienda kuombaomba mawe ya kujengea, ingawa hakuwa na uzoefu na kazi nzito namna hiyo.

1208 Siku moja wakati wa Misa alisikiliza sehemu ya Injili ambayo Yesu aliwatuma kwa mara ya kwanza mitume wake (Mt. 10:7-10); hapo akaenda kwa padri kupata tafsiri zaidi na maelezo yake, halafu kwa shangwe akaanza kutekeleza, kwa kutupilia mbali mkanda na viatu, akavaa kanzu ngumu na kamba na kuhubiri toba. Kama siku hiyo, ambapo hatimaye alielewa wito wake, akaendelea daima kuwa mtu wa Injili na mwana wa Kanisa. Tarehe 16 Aprili, baada ya kuhubiri alifuatwa na ndugu Bernardo wa Quintavalle na labda ndugu Petro Cattani pia walioamua kujiunga naye; basi akawaongoza kanisani, wakasoma Injili kwa kufungua kitabu mara tatu, wakauza mali zao zote ili kuwagawia maskini kufuatana na waliyoyasoma: ndio mwanzo wa jamaa. Tarehe 23 Aprili ndugu Egidi pia akajiunga nao, na mara wakatawanyika wawiliwawili wahubirie mikoa ya jirani. Ndipo wafuasi walipoongezeka na mwishoni mwa mwaka walifikia kuwa wanane.

1209 Kisha kurudi Asizi wanne wengine wakajiunga nao: hapo wakaamua waende wote Roma ili kupata kibali cha Papa Inosenti III kusudi wawe na hakika ya kuwa maisha yao yanampendeza Mungu, na waeleweke kwa wote kuwa ni Wakatoliki hasa, si wazushi. Baada ya kuvumilia muda fulani wakafaulu kuongea na Papa kwa msaada wa askofu wa Asizi na wa kardinali Yohane wa Mtakatifu Paulo. Mara ya kwanza makardinali wengine walitaka kupinga ombi hilo; lakini mara ya pili Papa alitoa kwa sauti kibali chake kwa maisha yao ya kitawa na kwa utume wao wa kuhubiri toba. Labda mwaka huohuo Fransisko alianzisha utawa maalumu kwa waamini wanaoishi katika mazingira ya kawaida ya ulimwenguni, waweze kufuata maisha ya Kiinjili kwa ukamilifu mkubwa zaidi.

1210 Jamaa, baada ya kuhama kibanda cha Rivotorto ili kukwepa ugomvi na mkulima mkorofi, walihamia moja kwa moja kwenye kanisa la mtakatifu Maria wa Malaika, ambapo palitakiwa kubaki kielelezo cha kudumu.

1211 Fransisko akaondoka kwa meli aende Sirya akawahubirie Waislamu, lakini safari ikaishia Korasya kutokana na dhoruba; hapo akarudi Italia.

1212 Usiku baada ya Jumapili ya Matawi mtakatifu Klara alitoroka nyumbani, akapokewa na Ndugu Wadogo kwa mienge, akanyolewa kitawa na Fransisko akavikwa kanzu. Baada ya muda akahamia kwenye kanisa la mtakatifu Damiano pamoja na mdogo wake mtakatifu Anyesi aliyemfuata utawani: ndio mwanzo wa utawa wa Mabibi Fukara, ambao wanaishi Kifransisko katika sala na kazi za mikono, bila kutoka wala kufanya utume nje ya monasteri.

1213 Fransisko alifunga Kwaresima nzima katika kisiwa cha ziwa Trasimeno, halafu akazawadiwa mlima La Verna.

1214 Fransisko aliondoka tena kupitia bara akawahubirie Waislamu wa Moroko, lakini akiwa njiani huko Hispania akapatwa na ugonjwa mkali akarudi Asizi, alipowapokea utawani wasomi kadhaa: baadhi yao wakashika kweli njia ya udogo, lakini wengine wakaja kuvuruga utawa kwa kutegemea mno akili yao.

1215 Mnamo Novemba ulifanyika Mtaguso Mkuu IV wa Laterano, ambao Fransisko aliweza kuhudhuria pamoja na maaskofu na wakuu wengine wa mashirika; labda ndipo alipofunga urafiki na mtakatifu Dominiko, mwanzilishi wa Utawa wa Wahubiri. Baadaye akajitahidi sana kutekeleza maagizo ya mtaguso huo.

1216 Siku mbili baada ya kifo cha Inosenti III makardinali walimchagua Papa Honori III. Fransisko aliendelea kuzungukazunguka Italia kwa ajili ya utume.

1217 Mkutano mkuu wa Ndugu Wadogo ulipoamua wengine waende kuhubiri nje ya Italia kwa Wakristo na wasio Wakristo, Fransisko akaelekea Ufaransa lakini njiani akazuiwa na kardinali Hugolino akarudi Asizi. Kwa kuwa walitumwa bila maandalizi yoyote, ndugu wengi wakapatwa na matatizo mengi.

1218 Honori III alisambaza hati yake maalumu ili kuwahakikisha maaskofu wote kuwa Ndugu Wadogo ni Wakatoliki hasa.

1219 Mkutano mkuu ulituma tena ndugu wakahubiri Injili kwa Wakristo na Waislamu. Fransisko mwenyewe akaenda kati ya Waislamu wa Misri: hakupenda mwenendo wa jeshi la Kikristo lililopigana nao, akatabiri kuwa watashindwa. Upande wake akaenda kumhubiria sultani, lakini kisha kuona hawezi kumuongoa wala kuuawa naye kishahidi akamuomba ruhusa ya kutembelea mahali patakatifu pa Palestina na Sirya.

1220 Tarehe 16 Januari huko Moroko Waislamu waliwaua ndugu Berardo na wenzake wanne waliokwenda kuwahubiria mpaka misikitini: ndio wafiadini wa kwanza wa Kifransisko. Mnamo Aprili au Mei Fransisko, alipopashwa habari za mageuzi ndani ya shirika, akarudi Italia kwa ufunuo wa Mungu ashike tena uongozi. Alipoona ugumu wa hali ya utawa, na kwamba wengi hawataki kumsikiliza tena, akamuomba Papa alipatie shirika kardinali Hugolino kama msimamizi na mkosoaji. Halafu katika mkutano mkuu akajiuzulu akamteua ndugu Petro Cattani aongoze jamaa kwa niaba yake.

1221 Kwa kuwa Petro Cattani kafa mapema tarehe 30 Mei ikambidi Fransisko amchague makamu mwingine, yaani ndugu Elia Bombarone, wakati wa mkutano mkuu ambao ulihudhuriwa na wanashirika elfu tano. Kutokana na wingi huo walijitengenezea vibanda vya mikeka, hivyo mkutano huo, mkubwa kuliko yote hadi leo, unajulikana kama mkutano wa mikeka. Mungu alifanya wasikose chakula hata wengi wakashangaa kwa sababu hayakufanyika maandalizi yoyote. Pamoja na kuamua kupeleka ndugu katika nchi mbalimbali, mkutano huo ulipitisha kanuni ndefu iliyohitajiwa sana na hali ya shirika, na hasa ongezeko hilo la ajabu. Lakini kanuni hiyo haikuthibitishwa na Papa kwa sababu fulani.

1222 Fransisko alizunguka sana Italia kwa ajili ya utume.

1223 Miezi ya kwanza alikwenda pamoja na ndugu Leo na ndugu Bonisyo kwenye mlima wa Fonte Colombo ili kuandika kanuni fupi na yenye mtindo wa kisheria zaidi kama alivyodaiwa. Upinzani wa ndugu Elia na wengineo ukashindwa katika mkutano mkuu wa Juni, hivyo kanuni ikapelekwa kwa Honori III ambaye akaithibitisha kwa maandishi tarehe 29 Novemba. Katika Misa ya usiku wa Noeli, iliyoadhimishwa huko Greccio katika pango lililoandaliwa na Fransisko, alitokea mtoto Yesu.

1224 Mnamo Julai ndugu Elia alijulishwa katika njozi kwamba Fransisko ataishi bado miaka miwili tu. Mnamo Agosti Fransisko akapanda mlima La Verna afanye mfungo mpaka sikukuu ya Malaika mkuu Mikaeli; huko upwekeni, akiwa katika malipizi na majaribu makali ya usiku wa roho, akatokewa na Yesu mwenye sura ya serafi msulubiwa akajaliwa mwilini madonda yake matano ya msalabani.

1225 Baada ya kurudi kutoka safarini mnamo Machi Fransisko alienda kwa mtakatifu Klara, ambapo akabaki mpaka Mei kwa sababu ya ugonjwa na ya matibabu yasiyomsaidia kitu. Katika mateso hayo na majaribu ya Shetani, usiku mmoja akaahidiwa uzima wa milele. Kesho yake asubuhi akamshukuru Mungu kwa kumtungia Wimbo wa Ndugu Jua. Mnamo Juni akawapatanisha askofu na meya wa Asizi kwa kuwaimbishia wimbo huo baada ya kuuongezea ubeti kuhusu msamaha. Halafu akaenda kukaa Rieti kwa ajili ya matibabu mbalimbali aliyoyavumilia yote kwa moyo mkuu.

1226 Kuanzia tarehe 6 Februari Fransisko alisafiri tena kwa matibabu. Mnamo Aprili akazidiwa huko Siena hata usiku fulani alikubali ombi la kuwaandikia ndugu zake wote wasia mfupi kwa maneno matatu, yaani kwamba wapendane, wafuate ufukara na kulitii Kanisa. Baada ya kupata nafuu akaandika sehemusehemu wasia mrefu zaidi ili kuchochea karama ya shirika. Waasizi wakiogopa kwamba mtakatifu wao atakuja kufa mbali wakafanya mpango wa kumrudisha kwao wakamlaza kwenye nyumba ya askofu. Lakini Fransisko alipokaribia kufa akaamua kurudi kwenye kanisa la mtakatifu Maria wa Malaika. Katika hiyo safari yake ya mwisho, katikati ya njia, akabariki mji wake. Halafu kabla hajafa akawabariki wafuasi wake wote, hata wale watakaoingia utawani mpaka mwisho wa dunia. Halafu tena akaomba wamlaze ardhini kabisa bila nguo afe uchi kama Yesu msalabani. Ikawa hivyo jioni ya tarehe 3 Oktoba; hapo sifa ya madonda yake ikaanza kuenea, na wengi wakaja kuyashuhudia katika maiti yake. Kesho yake, kwa maandamano ya shangwe pamoja na huzuni, akaenda kuzikwa katika kanisa kuu, lakini njiani waliwapitia mtakatifu Klara na wenzake.

1227 Tarehe 19 Machi, baada ya kufa Honori III, kardinali Hugolino alichaguliwa kuwa Papa kama alivyotabiriwa na Fransisko akajichagulia jina la Gregori IX.

1228 Mwenyewe alikwenda Asizi kusudi amtangaze rafiki yake Fransisko kuwa ni mtakatifu mbinguni (16 Julai).

1230 Masalia ya Fransisko yalihamishiwa katika kanisa kubwa lililojengwa kwa heshima yake: ndio kanisa kuu la shirika lote.

## SURA YAKE: taz. 1C 83

## 1. NGUZO ZA MAISHA YAKE

Maisha ya Fransisko yaligawanyika sehemu mbili: kilichozitenganisha ni kukutana kwake na Yesu mteswa katika wakoma (Test 1-3). Katika mateso yake, alitambua upendo wa Mungu ulivyo na jinsi usivyopendwa na watu. Ndiyo sababu alitaka kuuitikia, na kufuata nyayo za Yesu kikamilifu ili arudishe upendo kwa upendo. Kwa ajili hiyo alizidi kutafakari Injili inayomtambulisha pamoja na maisha na mawazo yake. Lakini Fransisko alifanya hivyo kwa kutegemea msaada wa mama Kanisa, tofauti na wazushi wengi wa zamani zile. Ndizo nguzo za maisha yake.

### 1.1. HAMU YA KULINGANA NA KRISTO

Fransisko alimtambua Yesu kuwa yule ambaye Mungu ameumba vyote kwa njia yake na kwa ajili yake, ambaye Baba amependezwa naye hata kwa njia yake ametutendea mema yote (ER XXIII,3-5; Adm V,1). Kadiri alivyozidi kuambatana naye alibandukana na ulimwengu (1C 13; 2C 211).

#### 1.1.1. MVUTO WA UBINADAMU WA YESU

Fransisko alimuonea kiu Yesu (2C 94) na kuunganika naye daima (1C 84; 115; AP 46; LMj IX,2), kiasi kwamba kutaja au kusikia jina lake kulikuwa sababu ya furaha kubwa kwake, si rohoni tu bali ilikuwa ikifurika nje na kuonekana kabisa (1C 82). Alikuwa akimuona katika mafukara na wagonjwa (AC 114; 2C 83), katika wanyama, wadudu na maua (1C 77; 79-81; 2C 111). Upendo kwa Yesu ulimsukuma kumuiga katika yote hata akaitwa Kristo mwingine (LtOrd 50-52; Adm VI; TestCl 5).

#### 1.1.2. HISANI KWA MTOTO YESU

Kati ya sikukuu zote alikuwa akifurahia Noeli kwa sababu ya kumpenda mtoto Yesu, Neno aliyetwaa udhaifu wetu; alitaka siku hiyo viumbe hai wote wapewe chakula cha pekee na kuta zisizoweza kula walau zipakwe damu (AC 14; 2C 199-200). Kipindi chote cha Noeli alikuwa akisali mara nyingi zaburi maalumu aliyoitunga mwenyewe (OfP XV). Kwa ruhusa ya Papa alianzisha mtindo wa kukumbuka usiku wa Bethlehemu kwa kutengeneza pango; alipofanya hivyo karibu na kijiji cha Greccio, wakati wa Misa mtoto Yesu akatokea penye majani ya hori (1C 84-87).

#### 1.1.3. HURUMA KWA YESU MSULUBIWA

Tangu ujanani Fransisko alimpenda Yesu msulubiwa (2C 109; 3C 2). Ndiyo sababu alisali sana mbele ya picha yake (PrCr) hata akasikia sauti kuitoka na kumtuma arekebishe Kanisa (L3C 13-14; 2C 10-11). Pia alitokewa na Yesu msulubiwa akawa akitoka machozi na kulia hata njiani akikumbuka mateso yake kama kwamba yangekuwa yake (L3C 14-15; AC 78; 2C 127; LMj I,5). Alipovikwa na askofu joho la fukara alilitia ishara ya msalaba (LMj II,4), halafu alichagua kanzu yenye sura ya msalaba (1C 90) na kutia saini kwa kutumia alama ya tau ambayo ni aina ya msalaba (3C 3). Karibu mwaka mzima alikuwa akisali zaburi za mateso alizozitunga mwenyewe ili kumtafakari Yesu (OfP; LCl 30): kabla ya kulala, akiteseka bustanini; usiku wa manane, akihojiwa na kudhihakiwa; asubuhi, akiwa mbele ya Pilato halafu akihukumiwa; adhuhuri, akisulubiwa, halafu akifa; hatimaye jioni akifufuka na kutawazwa. Yeye na wenzake walipokosa vitabu, badala yake walikuwa wakisoma msalaba usiku na mchana (LMj IV,3). Alikuwa akiuzungumzia mfululizo, na alipokaribia kufa alikiri hahitaji tena vitabu, kwa kuwa amemjua Kristo fukara msulubiwa (2C 105). Kutokana na hayo yote kwenye mlima La Verna akajaliwa kuungana

kikamilifu na mateso ya Bwana kwa kutiwa mwilini madonda yake yote matano (1C 94-95; L3C 17; LMj XIII,3), akaendelea kuwa nayo mpaka siku ya kufa (LMj XIII,5; XIV,1), ambapo wote waliweza kumuona akiwa kama kwamba ameshushwa kutoka msalabani wakati huohuo (1C 112-113; 117; LJS 71; 3C 4-5; LMj XV,2-3).

#### 1.1.4. IBADA KWA MWILI NA DAMU YA YESU

Kutokana na imani yake kwa ekaristi takatifu alimheshimu upeo Yesu hai katika sakramenti hiyo, hasa baada ya kuhudhuria Mtaguso Mkuu IV wa Laterano; katika maandishi yake karibu yote alihimiza wote waheshimu na kupokea vema mwili na damu ya Kristo (1L 3; 2LtF 14; 1LtCus 2-4; LtR 6; 2LtCus 4-5; LtOrd 12-13; Adm I; L3C 14), na hasa mapadri waadhimishe kwa usafi na shukrani (1LtCl; 2LtCl; LtOrd 14-33). Akiwaka upendo kwa mwili wa Bwana, alikuwa anaona ni kosa kutohudhuria Misa kila siku, akajitahidi kupokea mara nyingi kwa moyo wa ibada (AC 59; 2C 201). Alikuwa anamuabudu Yesu katika makanisa yote duniani (Test 4-5) na kufagia yale machafu (AC 60-61). Pia alitaka kutuma ndugu zake wakasambaze vyuma vizuri vya kuokea hostie, na sibori za thamani za kutunzia ekaristi (AC 108). Karibu na kufa alipenda kufanya ukumbusho fulani wa karamu ya mwisho kwa kugawa mkate alioubariki (AC 22).

## 1.2. MTINDO WA INJILI TAKATIFU

Fransisko, baada ya kuacha mtindo wa maisha aliourithi kwa mzee wake, yaani biashara, alianza kujitafutia mwingine (1C 16; Off 11:I-VI; LJS 11-14), lakini hakuridhika mpaka aliposikia jinsi Yesu alivyowapeleka mitume wake wakahubiri kwa ufukara (1C 22; LJS 15-16): ndio mtindo wa Injili takatifu alioushika moja kwa moja (Off 1:IV; AC 52).

#### 1.2.1. MTU WA KIINJILI

Alikuwa na imani na heshima kubwa kwa Maandiko Matakatifu kwa jumla, kiasi cha kuokota maandishi yoyote aliyoyakuta chini, akiogopa yana majina matakatifu au maneno ya Mungu (1LtCl 6-7; 2LtCl 6-7; 1LtCus 5; LtOrd 35-36; 1C 82; AC 108). Hasa alikuwa akijitahidi kukumbuka na kutafakari kwa upendo yale aliyoyasikia au aliyoyasoma katika Biblia (AC 79; 2C 102). Mbali ya kujua kwa moyo Injili karibu nzima alitamani kufikia ukamilifu kwa kuifuata kwa nguvu zake zote (LR XII,4; 1C 84; AC 52; 102; LMj V,1; XV,1) akajulikana na kuitwa mtu wa Kiinjili (HOcc 1-8; L3C 1; LMj Pr,1). Kila alipopatwa na wasiwasi kuhusu la kufanya, alisali ili kujua mapenzi ya Mungu akafungua Injili kwa imani na kusoma sehemu iliyotokea: ndivyo alivyofanya alipopata wafuasi wa kwanza (L3C 27-29; 2C 15), kuhusu vitabu vya binafsi (AC 104), kabla hajapata madonda ya Yesu (1C 92-93; LJS 60; LMj XIII,2) na karibu na kufa (1C 110). Hasa alijitahidi kuzingatia Injili ya Misa ya siku (InsL).

#### 1.2.2. KANUNI NI UTI WA INJILI

Fransisko alitaka wafuasi wake pia wawe watu wa Kiinjili (AP 37; LMj XI,1): ndiyo sababu akaandika kanuni mpya inayosisitiza Injili toka mwanzo hadi mwisho (ER XXII,41; LR I,1; XII,4; Test 14-15; AP 33; L3C 48-51; AC 102; LMj III,8-9; ChJG 15). Alifananisha kanuni hiyo, inayokusanya maneno mbalimbali ya Injili, na mkate mmoja uliotokana na vipande vingi vilivyounganishwa ili visipotee (2C 209; LMj IV,11). Kwa hiyo tena alikuwa akiita kanuni yake kitabu cha uzima, tumaini la wokovu, uti wa Injili, njia ya ukamilifu, ufunguo wa paradiso na ahadi ya agano la milele (2C 208). Kabla hajafa alionya wafuasi wake waweke Injili juu kuliko katiba yoyote (2C 216).

## 1.3. KUPENDA MAMA KANISA

Fransisko alitambua hawezi kuunganika na Kristo kwa kutengana na Mwili wake. Kwa hiyo alifanya daima kama siku ile aliyosikia Injili ya Yesu kuwatuma Thenashara mara ya kwanza: alitafuta maelezo ya padri asije akaenda tofauti na Kanisa. Ingawa wakati huo viongozi wake walikuwa na makosa mengi (1LtJV; ChJG 14), Fransisko alishika imani ya kwamba ndio waliowekwa na Yesu kulichunga Kanisa kwa Neno na sakramenti (Off 1:I; LJS 28).

#### 1.3.1. KUKAA DAIMA CHINI YA KANISA

Ili aongozwe kwa hakika katika njia ya Injili, Fransisko aliwahi kwenda kwa Papa na kukubaliwa naye kanuni yake (1C 32-33; ChRog 5-6; LJS 21; AP 31-36; L3C 62-63). Alitaka kabisa kufuata imani ya Kanisa la Roma na maagizo yake yote (ER II,12; LR II,2-5; 1C 62). Kwa hiyo alikuwa mkali sana kwa ndugu waliofanya kinyume (ER XIX,1-2; Test 31-33). Mwenyewe, kwa niaba ya ndugu wote pia, akaahidi kuwatii na kuwaheshimu daima Mapapa na hata kundi la Makardinali linaoliongoza Kanisa wakati hakuna Papa (ER I,3-4; LR I,2-3; L3C 52). Kwa kuwa askofu wa Roma ana kazi nyingi mno akaomba Kardinali mmojawapo auongoze utawa wake kwa niaba ya Papa (LR XII,3-4; 1C 99-100; L3C 64-67).

#### 1.3.2. KUTUMIKIA MAPADRI

Fransisko alikuwa akiwaheshimu daima mapadri, hata wale wakosefu zaidi, kama mabwana wake (2LtF 33-35; ER XIX,3; Test 6-10; Adm XXVI; 1C 9; AP 37; AC 58-59; 2C 8; ExSt), tena kuliko watakatifu wa mbinguni (2C 201). Aliwanyenyekea akisema ametumwa kuwasaidia kwa kuziba mapengo yao na kufidia makosa yao (AC 19). Alipotaka kuwahubiria, alikuwa akiwaita pembeni asije akawaaibisha mbele ya watu (AC 60). Lengo lake lilikuwa kuwaokoa hao pia pamoja na watu wao, kwa kukwepa wivu na kijicho na kwa kudumisha ushirikiano wa amani: ndiyo sababu alikataa daima kumuomba Papa ampe ruhusa ya kuhubiri hata askofu asipotaka (AC 20). Hivyo, akiingia eneo la jimbo au la parokia yoyote, kabla hajafanya mengine, alikuwa akienda kwa askofu au kwa paroko apewe ruhusa ya kuhubiri (1C 75; 2C 147). Kutokana na msimamo huo wa unyenyekevu na heshima, viongozi wa Kanisa kwa jumla wakampenda Fransisko na ndugu zake (1C 32; 99; AC 67) hata kumgongea kengele akiingia kwao (1C 62) na Makardinali wangetaka kuwa nao nyumbani (L3C 47-48; AC 117).

## 2. KARAMA YAKE

Kutokana na wito wa kulingana na Yesu ambao Mungu alimjalia Fransisko, maisha yake ya Kiinjili katika Kanisa yalikuwa na sifa maalumu, hasa kufanya na kuhubiri toba kwa udugu, udogo na furaha (CD; LCh 4-6; QA; ChRich 1).

### 2.1. ALIVYOTAKA WOTE WAWE MARAFIKI WA MUNGU

Tangu mwanzo Fransisko alishika maisha mchanganyiko: sala kwa wingi na utume mwingi (1LtJV; 1C 29; LJS 19-20; AP 15; 18; L3C 33). Usikivu kwa Roho Mtakatifu unahitajika sana ili pande hizo mbili ziwiane (HOcc 16-17): Fransisko ni mfano bora wa kuzioanisha na kupanga vizuri maisha ili muda wote ulete faida kwa sala au kwa utume (LJS 57; 59; LMj XIII,1).

#### 2.1.1. MTU WA KITUME HASA

Fransisko alivutiwa na maisha ya sala hasa akiona ubora na faida yake, lakini alijisikia vilevile haja ya kumtangaza Kristo ili awajulishe watu wote upendo wa Mungu, akaweka mbele ya hoja zote mfano wa Bwana Yesu aliyejitoa kabisa kwa wokovu wa watu (1C 71; 2C 172; LMj XII,1). Mara kadhaa alishawishiwa kuacha utume, akatafuta kujua mapenzi ya Mungu kwa njia ya wengine, halafu kwa utiifu akafuata mara mashauri yao akaenda kuhubiri (LMj XII,2) akaongoa watu wengi ajabu (LCh 9; L3C 26) na kubomoa ufalme wa Shetani (AC 108). Akizingatia jinsi Mwana wa Mungu alivyokubali mateso yote ili kuokoa watu, yeye pia kama rafiki yake halisi alifanya juu chini, akizungukazunguka miji na vijiji mpaka vinne au vitano kwa siku (1C 62; 65; 97). Aliposhindwa kutembea alidai atembezwe kwa punda ili ahimize watu kubeba misalaba yao (1C 98; LJS 64). Asipoweza kufika, aliandika barua mbalimbali (2LtF 2). Alihubiria hata ndege na viumbe vingine (1C 58; ChRog 7-8; ChRich 4; LCh 7). Alitaka ndugu zake pia wawake upendo kwa wokovu wa watu, ingawa mahubiri rasmi yatolewe tu na wale wanaojua vizuri mafundisho ya Kanisa, kadiri atakavyohakikisha mtumishi wa shirika lote (ER XVII,1-4; LR IX; AP 40; L3C 36; 59). Wengine watachangia utume wa jamaa kwa mfano wa maisha yao, kwa sala na sadaka (1LtF 8-10; 2LtF 51-53; LtOrd 5-9; HOcc 10-11). Tena kwa kila mmoja mahubiri yaendane na maisha mema hasa ya ufukara, unyenyekevu, upole na uvumilivu (1C 31; AP 38; L3C 58; AC 105). Kwa ajili hiyo hakutaka wafuasi wake wawe na makanisa makubwa, bali wakahubiri katika makanisa ya wengine kadiri watakavyoruhusiwa nao (QP; Test 6-7; 25-26; ChRog 1; AC 58; 2C 147). Vilevile alilaani wanaotoa makwazo hata kubomoa kazi ya Mungu na ya ndugu watakatifu (AC 59; 2C 156). Pamoja na kuheshimu watangazaji wa Neno la Mungu (Test 13), hakupenda tabia ya wale wanaohubiri ili kusifiwa, wakipamba tu hotuba zao badala ya kuzingatia moyo wa ibada na kujitafutia hekima kama lishe yao wenyewe (AC 47; 2C 163-164; 195; LMj XI,1). Alitaka hasa Neno la Mungu litangazwe kwa matendo mema (AC 20; 35-36).

#### 2.1.2. ALIYOYAHUBIRI

Tofauti na wafuasi wa rafiki yake Dominiko (JL; LivBr) waliokuwa watetezi wa ukweli wa imani katoliki, Fransisko aliwaelekeza Ndugu Wadogo wahubiri hasa namna ya kuishi Kikristo, yaani "vilema na maadili, adhabu na utukufu" (LR IX,3). Kwa neno moja Wafransisko wanatakiwa na Mungu wawahubirie watu wote toba (1LtCus 6-8; L3C 57), kusudi Kanisa lirekebike na ulimwengu uokoke (ER XXIII,7). Mambo hayo Fransisko aliwaruhusu ndugu wote wayahubiri kwa ufupi, hata wale wasiokubaliwa utume rasmi wa kuhubiri (ER XXI; AP 18-19). Mwenyewe alikuwa akiyahubiri kwa nguvu akitegemea utume aliopewa na Papa pamoja na ubora wa maisha yake (1C 33; 36; AP 36; L3C 53-54; LMj IV,1). Alijitosa vilevile kuhubiri kwa unyofu amani (1C 24; L3C 25) ili kupatanisha watu na Mungu (2C 155). Mtu wa amani, alifunuliwa awatakie wote amani hata katika kuwasalimu (ER XIV; Test 23; 1C 23; L3C 26; 37; AC 101). Amani hiyo ni tunda la toba, pia ni sharti la msamaha na wokovu wa Kimungu (AC 75).

#### 2.1.3. NAMNA YA KUHUBIRI

Kila mtu ana namna yake ya kuwasiliana na wenzake, lakini Fransisko alikuwa wa pekee zaidi. Kwanza, alipenda kuhubiri kwa maneno machache (LR IX,3). Pili, hakujiandaa kwa kusomasoma vitabu (Off 18:I-V), bali kwa kusali sirini ili moyo wake uwake upendo, asije akatoa maneno baridi (AC 103; 2C 164); kweli neno lake sahili lilikuwa la moto na kuwasha mioyo ya wasikilizaji wa aina zote (1C 23; 25; 36; ChRog 9; Off 15:VII-IX; BPr VI,8-13). Hakujali kama wasikilizaji ni wengi na maarufu au siyo, bali bidii zake zilikuwa daima zilezile (1C 72). Alikuwa hahubiri kama mapadri, bali kama raia katika mikutano yao, bila kupanga mfululizo wa mawazo (L3C 54; 2C 107; HSal). Alipojaribu kujiandaa katika nafasi za pekee, akaja kusahau hotuba hata ikambidi kukiri ukweli kwa aibu, lakini kisha kumuomba Roho Mtakatifu akajaliwa kugusa mioyo ya wote (LJS 58; LMj XII,7). Alijitahidi kueleza yasiyoelezeka kwa kutumia si ulimi tu, bali uso na mikono pia; pengine hata miguu ilikuwa ikichezacheza (1C 73) ili mwili wake wote useme (1C 97; 2C 191-192). Jambo la pekee katika kuhubiri kwa Fransisko na wenzake lilikuwa ni kuhubiri hata kwa vitendo na nyimbo ili wafikie si tu akili ya watu, bali moyo pia (2C 207; WBC XII). Mara nyingine badala ya kuhubiri au baada yake walikuwa na maigizo au kwaya, wakidai kama malipo si fedha bali matendo ya toba (AC 83). Matokeo ni kwamba watu wote walijitahidi kumuona na kumsikiliza (1C 36; ChRog 3-4; LJS 46; AP 8; HSal; LMj XII,12), wakaguswa sana na neema wakashika maisha ya Kikristo ulimwenguni na wengi utawani pia (1C 37; 56-57; 62; LJS 17-18; AP 41; L3C 27). Wasioweza kuacha ndoa na maisha ya kawaida walipewa naye mwongozo wa kufaa washike Injili kadiri ya hali yao: ndiyo asili ya utawa wa tatu kwa wasekulari (L3C 60; AC 8; 74; 2C 38; 3C 181; BPr VII).

#### 2.1.4. UMISIONARI WAKE

Fransisko alipokea agizo la Yesu la kwamba kila kiumbe kihubiriwe Injili: kwa ajili yake, na kwa lengo la kuwatia moyo wafuasi wake wenye dhiki, hakuogopa mateso wala kifo, bali alijitahidi kuwafikia Waislamu wa Sirya na Moroko mpaka akafaulu kuhubiri mbele ya Sultani wa Misri (6LtJV; HOcc 14-15; ChErn; 1C 55-57; ChBer;

ChRich 5; LCh 8; LJS 34-36; ChJG 10). Alielewa wazi kuwa Mungu aliwaita Ndugu Wadogo kwa wokovu wa watu wote na kuwa atawajalia mahitaji yao hata mbali na nchi za Kikristo (HOcc 13; AC 108). Kanuni yake ya kitawa ndiyo ya kwanza kuwa na sura nzima juu ya utume kati ya Waislamu na wengine wasio Wakristo (ER XVI; VD). Lakini hakupenda kulazimisha wafuasi wake wakakabili dhuluma, hivyo alitaka watumwe tu wanaojisikia na kukubaliwa (LR XII,1-2).

## 2.2. ALIVYOISHI KIDUGU

Yesu aliwafanya mitume wake kuwa kundi moja akawaambia, "Nyinyi nyote ni ndugu". Tofauti na wamonaki ambao alikuta wanaongozwa na abati (yaani baba wa kiroho), Fransisko alijenga utawa juu ya udugu wa Kiinjili akataka uwe jamaa tu (ER XIX,2; LR VIII,1; LtOrd 2; Test 33).

### 2.2.1. MAISHA YA UDUGU

Hasa mwanzoni kupokewa utawani hakukuwa kuingia nyumba fulani, bali jamaa na maisha yake (ER II,1-2; LR II,1; Test 16; L3C 35). Katika jamaa hiyo wote walikaribishwa bila ubaguzi (1C 31; BPr I), kutokana na imani ya kuwa Roho Mtakatifu anawashukia hata mafukara na wanyofu (2C 192-193). Fransisko alifurahia sifa mbalimbali za wafuasi wake (WSF 7) na kuwa na bidii kubwa kwa maisha ya pamoja (2C 208). Katika kanuni ya awali aliyaongezea maneno ya Injili taratibu chache zilizohitajiwa nayo (1C 32). Alitetea umoja hata kama gharama ya kuudumisha ni kuvumilia dhuluma za ndugu (Adm III,7-11). Kinyume chake, alichukia matendo ambayo yanakwaza watu na kuwaaibisha ndugu wema, akafikia hatua ya kulaani wanaojitofautisha na watawa wenzao (AC 59; 2C 156-157), hata kama ni kwa kisingizio cha utakatifu (AC 116; 2C 14; 32-33). Udugu unaonyeshwa na nguo pia, ambazo ni sawa kwa wote na kuwatambulisha kuwa shirika moja: si nguo za kiraia kama za mafukara wa kawaida bali kanzu yenye sura ya msalaba (1C 22; 24; 39; AP 14; 19; 41; L3C 27-29; 37). Ingawa ni duni, kanzu hiyo ina thamani kama ishara ya kuwekwa wakfu kwa Mungu; hivyo, makosa ya uzinifu na usengenyaji yanamfanya ndugu astahili kuvuliwa (ER XIII,1; 2C 116; 138). Udugu unaimarishwa hasa na sala za pamoja (LtOrd 30-31); hata wale wanaojitenga zaidi na ulimwengu kusudi wakazanie sala upwekeni wameagizwa na Fransisko waishi kidugu wao kwa wao (RH). Vilevile waliotumwa ulimwenguni kuinjilisha huko na huko (LMj IV,10) waende Kiinjili wawiliwawili (AC 108).

### 2.2.2. MIKUTANO YA KIDUGU

Ili kuimarisha na kuonyesha udugu wao, Wafransisko wanatakiwa kukutana kidugu kweli, si tu nyumba kwa nyumba, au mkoa kwa mkoa, bali pia kimataifa: awali walikuwa wakikutana wote mara mbili kwa mwaka, halafu ongezeko na tawanyiko la ndugu vikadai wapunguze mikutano na idadi ya wahudhuriaji (ER XVIII; LR VIII). Katika mikutano walikuwa wakiongea juu ya Mungu na juu ya maendeleo ya roho zao kwa kuzingatia hasa kanuni ya shirika (1C 42), ambayo kwanza waliirekebisharekebisha kwa pamoja (LtMin 13-21; 1LtJV). Kazi nyingine za mkutano mkuu zilikuwa uchaguzi wa mtumishi (LR VIII,2) na uenezi wa jamaa (HOcc 9; AP 40; LMj IV,10; ChJG 3; 17-19). Kimya na sala vilikuwa vikitawala pamoja na furaha ya kukaa kwa umoja, kiasi kwamba baada ya mikutano walikuwa wakitawanyika kwa huzuni ya kutengana, ingawa pia kwa hakika ya kuwa na ndugu wengi waadilifu (1C 38-39). Kilichowapendeza na kuwajenga zaidi ni kumuona mwenyewe na mwenendo wake (1C 29-30). Fransisko alikuwa akifurahi kuliko wote kwa jinsi alivyowapenda (LtL; 1C 51; AC 51; 90; 2C 172; 181). Alikuwa akiwapokea kwa unyenyekevu na baada ya kuwahutubia (AP 37-39; L3C 57-59; ChJG 16) alikuwa akiwabariki wote (BlL; AC 59). Alifanya vilevile kabla hajafa, baada ya kuwagawia vipande vya mkate, na kwa njia yao aliwabariki hata wale wa mbali na wale watakaoingia utawani mpaka mwisho wa dunia (1C 108-109; LJS 68; AC 22; 59; 2C 216-217).

### 2.2.3. UPENDO WA KIMAMA

Kila jamaa inajengwa na upendo, ndiyo sababu Fransisko alisisitiza ndugu wapendane kama mama na mtoto (ER IX,10-11; LR VI,7-8; AC 59), wawahurumie na kuwaombea wale wote waliokosa (ER III,5,10), wasioneane wivu, wala kugombana na kuhukumiana, bali wajihadhari na hasira au fadhaiko kwa dhambi yoyote (ER V,5-8; LR VII,3; LtMin). Kwa ajili hiyo alitumia mbinu zote aliondolee shirika lake masingizio na masengenyo ambayo ni kama tauni au sumu, na wanaoyasema ni chawa wanaouma (ER V,13; XI,4-12; LR III,10; Adm XXV; 2C 182-183; LMj VIII,4). Ndugu Wadogo waonekane watoto wa tumbo moja, katika kuchanga vitu vyote na katika kuelezana shida za kiroho pia (ER IV,4-5; VII,15; 2C 180; 191). Hasa Fransisko alitaka na kufaulu kufanya ndugu wa kwanza wawe kielelezo cha umoja na upendo (1C 41; 46; AP 25-26; L3C 43-44) kama mwenyewe (2C 172; 181; 214) aliyewaona wote kama zawadi za Bwana (Test 14; AC 107) na kuwaelekea kwa heshima zote (1C 83; AC 66). Pengine alikwepa kubishana nao asije akasababisha kikwazo (AC 101). Upendo huo ulienea kwa marehemu (ER III,6, 10; LR III,4) na kwa ukoo wa kila ndugu (AC 61; 93; 2C 91).

### 2.2.4. NDUGU WAGONJWA NA WAKOSEFU

Kati ya ndugu wote, Fransisko alipendelea wagonjwa akijua ugumu wa hali yao hasa katika mazingira yale ya kifukara. Kwa huruma alikuwa akiwaruhusu wasifuate sheria fulanifulani (ER VIII,3,7; 3LAg 31; AC 30; 2C 69; LCl 17-18; 31) hata akajiachilia kusudi wasipate aibu kula peke yao (AC 50; 53; 2C 22; 176). Akishiriki uchungu wao alikuwa akishughulikia mahitaji yao hata kuwaombea nyama na kuwafariji kwa maneno yake (AC 45; 2C 175). Alitaka wote wafuate mifano hiyo na kumshughulikia mgonjwa kama wanavyopenda kutunzwa wakiugua (ER X,1-2; LR IV,2-3; VI,9; Adm XXIV; AC 85). Mwenyewe alikuwa na shukrani kwa wauguzi wake na kwa njia hiyo pia alionyesha uzuri wa udugu (1C 102; AC 89). Upande mwingine alihimiza wagonjwa wavumilie maradhi na utovu wa mahitaji (ER X,3-4; CantExh 5-6; AC 45). Huruma kama hiyo alikuwa nayo kwa ndugu waliofanya kosa (2C 158) akiwahimiza wengine pia wawapende na kuwapokea (ER V,5-8; LR VII; LtMin 9-12; Adm XVIII,1; 2C 185). Hata hivyo, alikuwa na msimamo dhidi ya wanaorudiarudia makosa akawaadhibu ili kudumisha nidhamu (AC 107).

## 2.3. ALIVYOPENDA UDOGO

Fransisko, akizingatia unyenyekevu na ufukara wa Yesu (LR XII,4; Adm I,14-18), alipenda kushika udogo, yaani kujishusha kiroho na kijamii: ndiyo maana aliita watawa wake "Ndugu Wadogo" (HOcc 3; 1C 38; ChBur; ChAlb 1; LMj VI,5).

### 2.3.1 UDOGO WAKE

Kwa kazi yake alikuwa mdogo, na alama ya kuwa ndiye kiongozi wa wadogo ilikuwa kuwapita wote katika unyenyekevu (AP 37; L3C 57; AC 11; 2C 18; 139-140; LMj VI,1; ChJG 13). Alipenda kufuata maoni ya wengine kuliko ya kwake, akijidharau katika mawazo, maneno na matendo kwa kujiona kiumbe ambaye hafai wala kustahili neema alizozipata (1LtCus 1; 2LtCus 1; LtOrd 3; 47; 1C 53; 92; 142; AC 65; 109; 145; 2C 123). Alikuwa akificha kama siri neema za Bwana (2C 133), hasa zile za sala (2C 99; LMj X,4) na madonda matakatifu (1C 95; 2C 135-136). Baada ya kuanza kusifiwa na watu na kupata wafuasi wengi alijitahidi kukumbuka unyonge wake na kwamba bado anaweza akapotoka (AC 10; 2C 133). Alipenda kudharauliwa (AC 10; 2C 141), kuonywa (2C 142), kuungama wazi makosa yake hata ya mawazo, na kuomba msamaha mara moja (LtOrd 38-39; 1C 52; 54; LJS 33; AC 80-81; 2C 130-132; LMj VI,2). Akishindwa kukwepa sifa, alikuwa akimlazimisha ndugu mmojawapo amtukane, akipokea matusi kwa furaha na shukrani kama maneno yanayomfaa mwana wa Petro Bernardone (1C 53; 2C 130). Pia hakutaka kujivunia kifodini cha wanashirika (ChJG 8). Hasa baada ya kuacha uongozi wa shirika alikuwa akitii wafuasi wake (AC 39; 2C 143). Pamoja na kunyenyekea hivyo hakusita kulinda na kutetea kazi ya Mungu ndani yake na ya watu wake ili itimizwe kikamilifu (1C 33). Alikataza wasipotoshe maana ya maneno yake, hasa katika kanuni ya Ndugu Wadogo kwa kuwa aliipokea kwa Yesu (ER XXIV; LtOrd 40; Test 35-41; AC 17). Alisisitiza yazingatiwe na kunakiliwa na kutekelezwa, akitisha hata mapadri kuwa wataadhibiwa siku ya hukumu wasipofanya hivyo (1LtF 19-22; 2LtF 87; 1LtCl 13-15; 2LtCl 14-15; 1LtCus 9-10; LtR 8-9; LtOrd 47-49).

### 2.3.2. NJIA YA UDOGO

Mtakatifu wetu, pamoja na kufuata njia ya udogo, aliwaelekeza wafuasi wake njia hiyohiyo hata kwa majina aliyotaka wayatumie, kwa kuwa aliwakataza wasiitwe wakuu, bali ndugu wadogo kwa jumla; viongozi pia waitwe watumishi, watunzaji na walinzi, ambayo yote ni majina ya Kiinjili (AC 9; LMj VI,5). Katika mikutano mikuu ya shirika, akitoa mawaidha tunayoweza kuyasoma mpaka leo, alisisitiza mara nyingi unyenyekevu, akionya hasa ndugu wasijivunie mema wanayotendewa na Mungu bali wamrudishie yeye sifa zote (Adm XII; 2C 134) wasije wakafanya kama sanamu ambayo ingejisifia heshima ambazo kwa njia yake watu wanamtolea Bwana au mtakatifu fulani anayewakilishwa nayo (AC 10). Kadiri wanavyojaliwa neema wajinyenyekeshe kwa sababu palipo unyenyenyekevu pana maadili yote (SalV). Wafurahie mema ambayo Mungu anayatenda kwa njia ya wengine, kama vile yale anayotenda kwa njia yao (Adm XVII). Ndugu walio wadogo kwelikweli hawawezi kuhuzunika na kuacha nia ya kutafuta utakatifu kwa sababu tu wanadharauliwa na kukataliwa: wasijali sifa au lawama kwa kuwa hizo hazibadili hali yao mbele ya Mungu (Adm XIX,1-2). Alikataa katakata ndugu zake wasipate uaskofu wala vyeo vingine vya juu (AC 49; 2C 148; BPr V,1-7). Wajichagulie nafasi za mwisho, kazi duni na kukaa chini ya wote (ER XVII,5-18; 1C 38). Wafurahie na kupendelea waishi na watu wadogo na kuhusiana nao (ER IX,2), wakiwa wanyenyekevu kati ya watu wa chini kama vile kati ya wakuu (Adm XXIII,1).

## 2.4. ALIVYOISHI KWA FURAHA

Yesu alitaka wafuasi wake wawe na furaha kamili. Sifa mojawapo ya Fransisko inayotuvutia sana ni ile furaha ya moyoni ambayo iliweza kudumu hata katika mateso.

### 2.4.1. MTU WA FURAHA

Fransisko alikuwa mchangamfu kwa silika yake; lakini katika kumfuata Kristo furaha yake ilikomaa kabisa (L3C 4; 2C 4). Wakati wa kuongoka alikabili kwa furaha hata mateso yaliyompata kutoka kwa baba yake (1C 10; 13-14; LCh 2; L3C 7). Vilevile alipovamiwa na majambazi na kutupwa katika shimo la theluji, akazidi kumuimbia Mungu (1C 16; LJS 10). Kwa namna ya pekee alijaa furaha katika kuelewa na kufuata maisha ya Kiinjili aliyoitiwa (1C 7; 22; L3C 13). Kwa bidii yake yote alidumisha furaha ya rohoni na kukwepa huzuni (AC 120; 2C 125). Alipokuwa anashindwa, basi alikuwa akijitenga kidogo na wenzake asije akawaambukiza ugonjwa huo (AC 63). Kinyume chake alipenda kuonyesha furaha hasa kwa kuimba na kupiga ala za muziki (AC 38; 2C 127). Vilevile katika mateso alikuwa akitumia nyimbo na muziki kwa kujifariji, hata Mungu mwenyewe alituma malaika wake wamsaidie dawa hiyo (2C 126).

### 2.4.2. FURAHA YA NDUGU WA KWANZA

Fransisko aliwahimiza wafuasi wake wawe na furaha hiyo ya kiroho: wasifanane na wanafiki wenye kukunja uso, bali waonyeshe daima wanavyomfurahia Bwana, wakiwa wachangamfu na wenye kupendeza pasipo kukosa adabu ya kitawa (LR VII,16). Lengo kuu la kufanya hivyo ni kumzuia Shetani asipate nafasi moyoni kwa kuwa ni rahisi mwenye huzuni apatwe na mawazo mabaya dhidi ya wenzake, ya kukata tamaa au ya kutamani anasa (AC 120; 2C 125). Kwa hiyo alikuwa akilaumu ndugu wenye uso wa huzuni akiwashauri wazifikirie dhambi zao hata kwa kulia machozi chumbani, si mbele ya wengine (2C 128). Ndugu zake wa kwanza walifuata mashauri hayo kiasi kwamba mpaka leo wanaosoma habari zao wanafurahi (L3C 25-45).

### 2.4.3. FURAHA KAMILI

Fransisko anajulikana kama mtakatifu wa furaha kamili kwa kuwa aliweza kufafanua furaha hiyo inavyopatikana katika majaribu (TPJ; 2C 125; 145). Furaha yake hasa ni ile aliyojaliwa hata katika mateso makali ya mwili na roho (ER XVII,8). Kinyume chake alichukia porojo na maongezi ya bure, akataka ionekane wazi kwamba furaha ya mtawa ni katika maneno na matendo ya Bwana (Adm XX; AC 120). Alijifunza kujivunia udhaifu

wake na kuchukua msalaba kila siku (Adm V,4-8): mengine yote aliyaona si ya kwake, tena yanaweza yakageuka kizuizi, hata kama ni mazuri na ya kiroho. Furaha ilimzidi tena alipoambiwa na Bwana aache wasiwasi juu ya wokovu wake kwa kuwa atakwenda mbinguni tu (AC 83; 2C 217; WBC VI). Kwa hiyo ingawa maradhi yakazidi kumtesa akawa anaimbaimba sifa za Bwana mpaka saa ya kufa (AC 7; 99; 2C 214).

## 3. MPANGILIO WA UPENDO WAKE

Fransisko aliutambua upendo kuwa adili muhimu kuliko yote, akawa nao kwa kiwango kikubwa kufuatana na mpangilio wake sahihi.

### 3.1. KWANZA MUNGU

Nafasi ambayo Mungu anaistahili katika moyo na maisha ya binadamu ndiyo aliyopewa na Fransisko (AP 46), yaani nafasi ya pekee kabisa kama mwanzo na mwisho wa vyote alivyoviona mapema kuwa batili mbele yake (1C 3; 8; LJS 1-6; L3C 19).

#### 3.1.1. ALIVYOMPENDA MUNGU BABA

Fransisko akimtazama Mungu kwa imani alimtambua kuwa Baba mwema (2C 12; L3C 20; LMj II,4) anayestahili kupendwa na kusifiwa (2LtF 18-21; ER XVII,17-19; XXII,27-31). Wakati kuna watakatifu wanaofurahia mwanga wake unaoangaza akili, Fransisko aliguswa zaidi na upendo wake wa Kibaba (1LtF 11; 2LtF 54; AC 90; 2C 196; LMj IX,1) na wema wake mkuu unaovutia utashi umpende kabisa (ER XXIII; PrOF 5; PrsAH). Sala zake tulizonazo zinaonyesha wazi alivyoonja wema wa Mungu (PrsG). Alikiri kwamba binadamu hastahili kumtaja Muumba wake, ambaye mbingu na dunia zinatakiwa kuliinamia jina lake takatifu (1C 82; L3C 68; LMj X,6). Hivyo alitaka kushirikisha viumbe vyote katika sala ya sifa na kuwasha mioyo ya watu wote wamuabudu Mungu inavyowapasa (2LtF 61-62; 1LtCus 8; LtR 7-8; CtC; LCh 8; AP 15; 2C 213; 217). Tangu mwanzo wa uongofu wake, namna yake ya kusali ilivuta watu, kama ndugu Bernardo aliyemsikia usiku kucha akilia machozi na kusema, "Mungu wangu, Mungu wangu" (1C 24; 26). Aliwafundisha ndugu zake kusali usiku (RH; 1C 47; AP 25) na kutulia kwa ndani kwa sala na tafakuri (ER VII,12; XXII,27-32; LR X,8-9; 1C 40; 43; 45; LMj IV,3), akisema roho isipotulia hivyo mwilini, basi chumba cha binafsi (RH) hakiwezi kumsaidia mtawa (AC 107-108). Pia aliwaagiza wasali kila siku Baba Yetu mara nyingi (LJS 27) au Sala ya Kanisa la Roma kwa nia ya kumpendeza Mungu, si watu wanaosikia (RH 3-6; ER III,3-10; LR III,1-4; LtOrd 40-44; Test 18; 29-33; AC 103; InsL). Alikubali mtakatifu Antoni wa Padua afundishe teolojia, lakini kwa sharti la kwamba roho ya sala isizimike (LtAt) kama kanuni ilivyokwishasema kuhusu kazi nyingine (LR V).

#### 3.1.2. MTU WA SALA

Kwa jinsi alivyovutiwa na wema wa Mungu, Fransisko alishika sana maisha ya sala (1C 71; 103; AC 59; 83; LMj X,1) na kuyafanikisha kwa mbinu mbalimbali: penye nia pana njia. Waliomfahamu walishuhudia alivyopenda kuungana na Mungu, akimjibu kama hakimu, akimlilia kama Baba, akiongea naye kama rafiki, akimfurahia kama bwanaarusi, hata akageuka kuwa sala (2C 95). Alikuwa akitumia muda wake, sehemu katika kupanda juu kwa Mungu na sehemu katika kusaidia watu bila kumsahau mpenzi mkuu (LR V,1-2; LtAnt; 1C 91; 2C 185; LMj XIII,1). Ilikuwa kawaida yake kusali vipindi vyote vya Sala ya Kanisa kwa wakati wake, bila haraka, huku amesimama, asijali hata mvua iliyomnyeshea katika kulisha roho yake chakula ambacho ni Mungu mwenyewe (AC 120; 2C 45; 96). Kabla ya Sala ya Kanisa alikuwa akijiandaa kwa masifu fulani aliyoyatunga kwa moto wa upendo wake (PrsAH). Aliongea na Mfalme mkuu kwa bidii nyingi asishikwe na mawazo mengine; na alipotambua kitu kilichomzuia asifanye hivyo, alikuwa tayari kukiondoa kabisa (2C 97). Alikuwa akijitafutia mahali ambapo aweze kuungana na Mungu wake si kwa roho tu, bali kwa viungo vyake pia (1C 10; 91; AC 65; 2C 35): upwekeni alikuwa akisujudu (2C 10) au kusali kwa sauti kuu na kutoka machozi, kunyosha mikono (2C 46) na kujipigapiga kifua (LMj X,4). Alikataza kabisa watu wasimuendee huko wasipoitwa kwanza (AC 73; 2C 100). Kwa kuwa alizoea utamu wa Kimungu hakuyapenda tena yale yanayowapendeza watu wa ulimwenguni (1C 103); basi, alikuwa anakatisha maneno ya wageni wake arudi upwekeni (2C 94). Ikiwa neema ya pekee ilimfikia kwa dharura akiwa kati ya watu (L3C 8; 2C 167), basi alifanya bidii abaki peke yake (2C 95) au kujifunika uso (2C 94), ingawa pengine alijisahau kabisa kwa kuzama ndani ya Mungu (2C 98; LMj X,2). Lengo la kutafuta upweke halikuwa akimbie matatizo ya maisha, bali aweze kumsifu Mungu, kujua mapenzi yake na kuombea watu (LMj X,3). Alikuwa anaomba kujua matakwa ya Mungu, aweze kuyatimiza kama mtumishi mwaminifu (PrCr; 1LtF 9; 2LtF 52; ER XXII,9; LtOrd 50-52; 1C 6; 107; AC 6; 63; 108; 118). Sala yake ilikuwa pia ya maombezi, hasa kwa ajili ya utawa wake (AC 112; 2C 68; 143; LMj IV,10; XI,11) na ya wakosefu ambao aliwaombea kwa machozi (AC 76; 112; 2C 101; LMj X,4). Kutokana na sala alijaliwa kujua mengi yaliyofichika (1C 47-48; LJS 29-31; 2C 13; TestCl 6-17; LMj IV,4; WBC III; IV; XI; XII) pamoja na kuahidiwa na Bwana kwamba utawa wake hautakoma bali utakuwa baraka kwa wale wote ambao wataupenda na kuutetea (WSF 6).

#### 3.1.3. KUMTEGEMEA BABA

Fransisko alikuwa na hakika juu ya upendo wa Mungu, hivyo alimtegemea kabisa maisha yake yote (1C 10; AC 40; 2C 144). Hakushughulikia mahitaji yake ya kidunia, wala kukubali ndugu wahangaikie ya kesho (AC 52), ingawa watu wengine walidhani hana busara, kwa mfano alipokataza maandalizi yoyote kwa mkutano wa mikeka walipokusanyika ndugu elfu tatu (ChJG 15-16). Upande wake Mwenyezi Mungu alimuongoza daima kama Baba (1C 3-6; AP 6; L3C 6; 2C 10), akitekeleza mapema maombi na matazamio yake, akimjalia mara nyingi kwa namna ya ajabu yale aliyoyahitaji pamoja na wenzake (HOcc 12; 1C 34; 55; AC 8; 68; 2C 44; 3C 33; 15; 36; BPr VI,33-37). Katika njia ya udogo Fransisko aliombaomba mahitaji yake na ya wenzake, akijua kwamba asipojitegemea atajifunza kumtegemea Mungu. Akikumbuka ufukara wa Yesu na kwa upendo wake, hata kabla hajaongoka

aliombaomba huko Roma kwenye kanisa la mtakatifu Petro (L3C 10; 2C 8; LMj I,6). Halafu akakataa chakula alichoandaliwa na padri wa kanisa la mtakatifu Damiano, akapitia Asizi mlango kwa mlango kuombaomba chochote kile na kula mabaki mbalimbali ya walichokula watu (L3C 22; 2C 14; LMj II,7). Ingawa mwanzoni ilimbidi ajikaze, baadaye akapendelea kufanya hivyo kuliko kupewa bila kuomba (2C 71). Vilevile alikuwa akiombaomba kwa raia au kwa wanashirika katika sikukuu (LMj VII,8-9) na katika nyumba jirani na ile alipoandaliwa karamu, akiona afadhali kufuata ufukara wa Yesu kuliko adabu njema (AC 96-97; 2C 72-73). Lakini alisisitiza pia ndugu wafanye kazi, wasiombe wala kutumia misaada mingi kuliko mahitaji, wasije wakawaibia mafukara wengine sehemu yao (AC 15; WSF 1). Mwanzoni aliwaonea huruma wanashirika wenye aibu katika kuombaomba, lakini baadaye alitaka hata wahubiri na wenye kazi nyingine katika shirika wasikae muda mrefu bila kwenda kuombaomba kwa furaha, wakijua ndiyo haki ya mafukara (RH 5; ER VII,8; IX; LR VI,1-6; Test 22; 1C 34; AC 97-98; 103; 2C 76). Aliwaeleza kwamba kwa kazi hiyo wanawapatia wafadhili tuzo la Mungu lenye faida kuliko kama wangewalipa (AC 51; 2C 71; 74)

## 3.2. HESHIMA KWA BIKIRA FUKARA, MALAIKA NA WATAKATIFU

Fransisko alikuwa Mkatoliki hasa, hivyo baada ya kumuabudu Mungu aliwaheshimu malaika, watakatifu, na kwa namna ya pekee Mzazi wa Mungu, akitaka pia kumshukuru Mungu na kuungama dhambi zake kwa njia yao (ER XXIII,6; LtOrd 38-39; Ant OfP).

### 3.2.1. UPENDO KWA MAMA WA YESU

Mwana wa Mungu alifanyika mwili kwa njia ya Bikira Maria (2LtF 4; ER XXIII,3; LtOrd 21; AC 14): kwa hiyo Fransisko alimpenda ajabu. Maandishi asili yanasisitiza heshima na upendo alivyokuwanavyo kwa Mama huyo, hata akamchagua kuwa mlinzi wa utawa wake (1C 24; 2C 198). Jambo hilo ni wazi katika maandishi yake, hasa katika sala ya kumuamkia Bikira Maria (SalBVM) na katika antifona ambayo alikuwa akiitumia mara 14 kwa siku (OfP). Alimuonyesha heshima yake hasa kwa kumuiga: kufuatana na karama yake alinuia kushika ufukara pia kwa kukumbuka shida zilizompata Mama wa Yesu (2LtF 5; ER IX,5; UltVol; 2C 67; 83; 85), akatoa machozi ya uchungu alipoukumbuka ufukara huo (2C 200). Kutokana na upendo wake kwa Bikira Maria wa Malaika alitengeneza kanisa lake katika bonde chini ya Asizi (1C 21), halafu akafurahi sana kulihamia alipopewa na Wabenedikto, akisema pale Porsyunkula panapendwa na Mama wa Mungu kuliko popote pengine na panatembelewa sana na malaika (1C 106; AC 56; 107; 2C 19). Mwanzoni mwa utawa alitaka mkutano mkuu ufanyike pale (ER XVIII,2), na mwisho akapenda kufia na kuzikwa palepale alipofunuliwa njia ya Injili na alipoendelea katika utakatifu (1C 108; AC 67; ChJG 50). Aliagiza paendelee daima kuwa mfano bora kwa jumuia zote duniani, ili wengine wakitaka kupotoka wajirekebishe watakapohiji pale au kusikia habari zake (AC 56).

### 3.2.2. HESHIMA KWA MALAIKA NA WATAKATIFU

Aliwaheshimu kwa upendo malaika kwa kuwa wanatupigania na kutulinda: kwa namna ya pekee alimheshimu mkuu wao, Mikaeli, akijiandaa kila mwaka kuadhimisha sikukuu yake kwa mfungo wa siku arubaini (2C 197): ni. wakati wa Kwaresima mojawapo ya namna hiyo, aliyoifanya kwenye mlima La Verna, kwamba alijaliwa madonda ya Yesu. Kuhusu watakatifu aliwaka moto wa Kimungu alipowakumbuka hao walio kielelezo kwetu (2C 202): kati yao alimheshimu zaidi Yohane Mbatizaji, aliyepewa jina lake katika ubatizo (2C 3), halafu mitume Petro na Paulo ambao alijiandaa kuadhimisha sikukuu yao kwa Kwaresima nyingine ya hiari (LMj IX,3). Alitamani kuiga watakatifu, hasa wafiadini (Adm I,19-21; LMj IX,5). Kinyume chake alilaumu wanaojisifia watakatifu wao wasijitahidi kuwaiga (Adm VI,2-3).

## 3.3. KILA MTU NI NDUGU

Kwa kumuamini Mungu kuwa Baba wa wote, Fransisko alitambua watu wote kuwa ndugu zake, akawapenda bila kumbagua hata adui (2Ltf 7; LR X), ila aliwapendelea mafukara (1C 76; 3C 173).

### 3.3.1. HAKUMBAGUA YEYOTE

Fransisko aliheshimu na kusaidia wenzake hata kabla hajaongoka (1C 17; AP 4; L3C 3; 9; 2C 5; LMj I,2). Kisha kujaa upendo wa Kristo, alisisitiza heshima kwa wote katika mawazo, maneno na matendo (ER VII), akitoa mashauri mbalimbali ya kufaa ili kutekeleza amri ya upendo (1Ltf 4; PrOF), kama vile kukwepa dharau (LR II; AP 38; L3C 58) na kijicho (Adm VIII), kuwa na huruma (Adm XVIII,1), kuvumilia (ER XIV; 1C 12), kukwepa hasira na fadhaiko kwa dhambi za watu (Adm XI), kutokwazwa nazo, kuacha matendo mabaya, kuwatendea mema watu wa aina yoyote, kutafuta faida ya wengine, si ya binafsi, kuwa na ukarimu, kuhisi shida za watu, kukubali kwa wema maombi yao, kukwepa matusi na kusamehe (PrOF).

### 3.3.2. ADUI PIA NI RAFIKI

Fransisko alijisikia ndugu wa wote asiweze kuona mwingine ni adui (AC 11). Akiwa kweli mtoto wa Mungu, alijitahidi daima kurudisha amani kati ya watu akihimiza wote kuvumilia na kusamehe (HSal; AC 84).Katika maendeleo ya Kiroho, alifikia na kuonyesha kilele cha upendo kwa kuona watesi kuwa marafiki na wafadhili wanaomsaidia kupata heri ya mbinguni (ER XXII); akisikitika kwa sababu wanatenda dhambi na kuchafua roho zao kuliko kwa usumbufu au uchungu wowote waliomsababishia (Adm IX). Kwa upendo huohuo aliona majambazi kuwa ndugu akawashughulikia kwa ukarimu na unyenyekevu kusudi waongoke, hata baadhi yao wakaingia utawani (L3C 58; AC 115).

### 3.3.3. FUKARA ANAMWAKILISHA KRISTO

Fransisko alipenda wote (AP 29; L3C 45), lakini kwa namna ya pekee mafukara, kwa sababu shida zao zinawafanya wafanane na Kristo. Hakuvumilia matusi wala lawama dhidi yao, ndiyo sababu alikuwa mkali na

kuadhibu ndugu waliowasema (LJS 45; AC 114; 2C 85). Alikuwa akisikitikia kumuona mtu fukara kuliko yeye, akiogopa atashindwa naye katika mashindano ya ufukara (1C 76). Upendo wake kwa mafukara haukuwa wa moyoni tu, bali ulitimizwa kwa matendo, hasa kwa kutoa msaada wowote ule (AP 27; L3C 43; LMj I,6) kama alivyonuia hata kabla hajaongoka. Kwa ajili yao alikuwa tayari kujinyima joho (AP 28; L3C 44; AC 31; 33; 89; 2C 86; 88; 92), kanzu au vitabu vya dini (LMj VIII,5), akiona afadhali kutimiza Injili inayoagiza upendo kuliko kuisoma tu (AC 93; 2C 91). Asipoweza kuwapa kitu aliwaonyesha huruma ya moyo wake. Alikuwa akiomba matajiri kwa ajili ya maskini, na kwa maandishi aliwahimiza waamini wote kutoa misaada ili kusafishwa madoa ya dhambi na kujipatia malipo mbinguni (2Ltf 5; AC 92). Kwa mtazamo wake maskini ana haki ya kupewa mahitaji: hivyo kumsaidia ni kumrudishia mali zake (AC 32; 2C 87). Kabla hajaongoka, kati ya watu wenye shida alikuwa akiwaogopa mno wakoma, hata akawakimbia kila alipowaona kwa mbali; kumbe baadaye akawa akiwatumikia kwa upendo wa pekee (1C 17; L3C 11) na kuwabusu na hata kula nao katika sahani moja (AC 64). Hata katika wasia wake alitia maanani mapinduzi hayo kuliko matukio mengine ya uongofu wake (Test 1-3; 1C 103; LMj XIV,1). Ndiyo maana aliagiza Ndugu Wadogo wote wafurahi kufanya hivyo, nao walelewe hasa kwa kufanya wajaribu kutumikia wakoma na kuishi kati yao (AC 9).

## 3.4. NDUGU WA VIUMBE VYOTE

Kabla ya Fransisko huko Ulaya ulienea sana uzushi wa kudharau vitu vinavyoonekana kama kwamba havikuumbwa na Mungu wetu mwema kwa kuwa eti, ni vibaya. Mungu alijibu kwa kumtokeza Fransisko, aliyevipenda kitakatifu viumbe vyote kuliko alivyofanya yeyote yule (Off 1:V). Hivyo bila kubishana na wazushi hao, alirudisha umati kukiri wema wa Mungu na wa kazi yake.

### 3.4.1. UPENDO WAKE KWA VIUMBE

Kwa kuwa upendo wake kwa viumbe vyote (1C 77) ulikuwa karama ya pekee yake binafsi, hakuna anayeweza kuuelewa wala kuueleza. Hata hivyo, mashahidi mbalimbali wametuandikia juu ya upendo huo wenye msingi wa imani hasa, kwamba katika viumbe alikuwa akitambua mara uwezo, hekima na hasa wema mkuu wa Muumba (2C 165; LMj III,6; IX,1). Kwa hiyo alikuwa akishangilia na kuhimiza wanyama, mimea na viumbe visivyo hai wamtukuze Mungu (1C 80), akiviita vyote ndugu na kuongea navyo kama kwamba vinamsikia (3C 31; LMj VIII,7). Alipenda ndege hata akawahubiria na kuwatengenezea viota (1C 58; LJS 37; AC 14; LMj XII,3). Alipenda zaidi wanakondoo ambao kwa upole wao ni mfano wa Yesu Kristo (1C 77; LJS 41): ndiyo maana mara nyingi aliwakomboa wasichinjwe (1C 79; LJS 42-43). Hata nyuki na wadudu wengine alikuwa akiwashughulikia wasije wakafa kwa baridi au kwa kukanyagwa (1C 80; LJS 44; 2C 165). Alipenda viumbe vingine pia hata asikate mti kwa namna usivyoweza kuchipua tena, asilime bustani ya mboga bila kuacha nafasi kwa majani mengine na maua (1C 81), wala asikubali kukanyaga maji na miamba bila heshima (AC 88; 2C 165). Alikuwa na upendo mkubwa ajabu kwa jua (1C 80; AC 83) na kwa moto hata asizime taa wala mshumaa, wala kujali unateketeza nini (AC 86-87). Basi alipohitaji kutibiwa kwa kuchomwa usoni alisema na moto na kumuomba Mungu usimuumize mno (AC 86; 2C 166; 3C 14; LMj V,9), ikawa hivyo. Kwa kufurahia kazi yote ya Muumba alimtungia “Wimbo wa Viumbe” (CtC; AC 83).

### 3.4.2. ALIVYORUDIA UTAKATIFU WA ASILI

Amani kati ya watu na wanyama, ambayo ilikuwepo mwanzoni ikatabiriwa na Isaya kuwa itakuwepo tena zamani za Masiya, ilionekana katika maisha ya watakatifu kadhaa, lakini hasa ya Fransisko (2C 166; 3C 14; LMj VIII,1). Akiwa mpole na mtiifu, alijaliwa wanyama wawe wapole na watiifu kwake (1C 59; 61; LJS 38-40; 2C 166; 3C 20; LMj V,6), kwa mfano tausi na vindege, sungura (1C 60; 3C 29-30; LMj VIII,8), vyura (BPr VI,30-32), samaki (1C 61), wadudu (2C 171; 3C 27; LMj VIII,9) na hata mbwamwitu (PasSV): ni kama kwamba alirudia utakatifu wa asili ambapo Adamu na viumbe vingine walikuwa jamaa moja. Viumbe mbalimbali vilimrudishia upendo (1C 59) kwa kumsikiliza kwa makini, kuitikia salamu yake, kumkaribisha mahali fulani, kumkaribia bila hofu, kusikitika katika kuachana naye, kumtumikia kwa uaminifu na huruma (2C 168; 3C 25; LMj VIII,10) na kushiriki katika kifo chake (3C 32; LMj XIV,6).

# 4. ALIVYOSHIKA MASHAURI YA KIINJILI

Fransisko akifuata mtindo wa Injili takatifu alipokea pia mashauri makuu matatu yaliyotolewa na Bwana kwa maisha na mafundisho yake. Ndiyo sababu jamaa aliyoianzisha ni utawa halisi, ingawa wa aina mpya (PD; CS; ChLau).

## 4.1. UPENDO WA MUNGU ULIMTOSHA

Fransisko ni mmojawapo kati ya watu waliotosheka na upendo wa Mungu wasihitaji mapendo ya kibinadamu katika ndoa (ER I,1; LR I,1). Uhusiano wake na wanawake uliridhisha na kufaa kwa usafi wa moyo ambao umwezeshe kumuona Mungu (ER XXII,27-31; Adm XVI).

### 4.1.1. UHUSIANO NA WANAWAKE KWA JUMLA

Kama walivyofanya wanaume wa koo mashuhuri wa wakati wake, Fransisko alikuwa na heshima ya pekee kwa wanawake: hivyo wengine wanasema hakuwahi kushindwa na tamaa katika uhusiano nao hata alipofuata anasa na vijana wenzake (LMj, Prol,2; I,1; BPr V,14-17). Kwa vyovyote baada ya kuongoka ushindi wake katika jambo hilo ukawa mkubwa kutokana na busara aliyotumia pamoja na kujitesa. Alikuwa akikubali kuongea nao kuhusu mambo ya kiroho tu, tena kwa ufupi na bila kuwatazama uso (2C 112; 114; LMj V,5). Alitesa viungo vyake ili

kutawala tamaa yoyote inayoweza kuchafua roho (LMj V,1). Pamoja na kujinyima sana hata vyakula, alikuwa akijipigapiga na pengine alijitupa katika maji baridi, theluji au miba (ER XXII,5; LMj V,3). Alisisitiza mara nyingi jinsi ilivyo rahisi hata kwa waadilifu kushindwa, hivyo mtu asijiamini akaacha tahadhari (2C 112; LMj V,5). Kwa kuwa Shetani haachi kushawishi ni lazima kusali asishinde hata baada ya miaka ya uongofu wala karibu na kifo (AC 37; 2C 113). Alihimiza sana ndugu wawe waangalifu na wanawake, kwanza kwa ajili yao wenyewe, halafu kusudi wasisababishe watu kuwa na shaka juu yao (ER XII; XIII; LR XI).

4.1.2. UHUSIANO NA KLARA, MABIBI FUKARA NA YAKOPA WA SETTESOLI

Kwa usafi huo aliweza kujengana kiroho na baadhi ya wanawake, hasa mtakatifu Klara ambaye ndiye mche wake wa kwanza katika utawa wa kike (1C 18-20; L3C 24; TestCl 37-38; RCl I,3-5; BCl 6-8; BC 5-8; LegCl 5-10; 24-26; LMj IV,6). Alikuwa na furaha akitembelea monasteri yake na kumfariji kwa mafundisho yake (TestCl 48-50). Waklara pia walipendwa sana na Fransisko katika Roho Mtakatifu aliyewaita kushiriki karama yake (2C 204). Aliona ingekuwa ukatili mkubwa kutowahudumia baada ya kuwaita utawani (CtExh; AC 85). Alikuwa akiwashughulikia sawa na ndugu wa kiume na kwa niaba ya hao pia akawaahidia kuwahudumia siku zote (FormViv; TestCl 24-33; RCl VI,1-5). Polepole aliacha kuwatembelea mara kwa mara pia kusudi awe mfano kwa ndugu zake (2C 205-207) kwa kuwa hakutaka waende kwa Waklara kwa hiari yao, ila watumwe kwa ruhusa ya Papa ndugu ambao hawapendi, tena wamejaribiwa kirefu utawani (LR XI,2; RCl XII,5-7). Lakini kabla hajafa aliwahimiza Ndugu Wadogo wawatimizie ahadi yake akawaandikia Waklara barua yenye baraka akitambua watashindwa kuonana kwa mara ya mwisho (AC 13; 109). Hao wote walimpenda sana mwanzilishi wao ilivyoonekana wazi walipoletewa maiti yake: walitokwa na machozi mengi kwa uchungu wa kufiwa lakini pia kwa faraja ya kuona madonda yake matakatifu (1C 116-117; LJS 72; AC 13; 109). Mwanamke mwingine aliyejaliwa upendo wake wa kidugu ni Yakopa wa Settesoli, mjane wa Roma aliyewahi kumkaribisha mara kadhaa nyumbani mwake; alipomtembelea Fransisko mahututi kutokana na njozi aliyojaliwa, aliruhusiwa naye kuingia chumbani alimolala na kumletea vitu alivyotaka kumuagiza, kumbe alivileta kabla hajapata ujumbe (AC 8; 3C 37-39). Mpaka leo kaburi lake liko jirani na lile la Fransisko pamoja na ya wenzake wa karibu zaidi.

## 4.2. ALIVYOISHI BILA MALI

Kwa binadamu yeyote viumbe vinaweza vikazuia uhusiano na Muumba, kwa kuwa vinaonekana wakati Mungu haonekani, tena vinamvutia avitumie visivyo. Fransisko alijaliwa neema hii pia, yaani kufurahia viumbe vyote, asitamani kuvimiliki hata kimoja: alivitumia kadiri vinavyohitajika tu huku akitambua na kutukuza wema wa Muumba wao. Hakushikamana na chochote cha duniani (LJS32) kusudi moyo wake uweze kuambatana kabisa na Mungu (1C 57; LMj IX,8) akajenga utawa wake juu ya ufukara mkuu (LJS 22; AC 102; TestCl 39-47; LMj VII,2).

4.2.1. AGANO NA BIBI UFUKARA

Fransisko tangu aongoke mpaka afe alijikatalia mali yoyote akashika ufukara kwa bidii ya pekee (LMj VII,1) akiuona ndio njia bora ya kumfuata Kristo na kufika mbinguni (2C 55; TestCl 56-57). Alisema ufukara ni adili la kifalme kwa jinsi ulivyong'aa katika maisha ya mfalme na malkia wetu (1Ltf 1; ER IX; UltVol; 2C 73-74; 200; TestCl 34-36; RCl VI,6-9). Alisikitika kufikiria ulivyoachwa na Wakristo, kwa kuwa wachache tu wanaelewa na kuchuma matunda yake (1C 3). Hivyo alijitahidi kuurudisha katika Kanisa na kuwa nao kuliko watu wote (2C 93; LMj VII,6), hata akawaonea kijicho wale tu waliokuwa fukara kuliko yeye, akiogopa watamzidi katika mashindano ya ufukara (2C 83; LMj VII,6). Kwa kuwa ulimwezesha kumfuata kabisa Mwana wa Mungu, aliupenda kama bibi (ScEx 56-69) au bibiarusi (L3C 7) akatamani kwa dhati aungane nao moja kwa moja akiwa mwaminifu kwake saa zote mpaka mwisho. Kwake ufukara ulikuwa ukombozi (1Ltf 11) na usafi wa moyo unaowezesha kumuona Mungu (Adm XVI) na kushinda uroho (Adm XXVII,3; SalV), mahangaiko ya maishani pamoja na ugomvi na watu (L3C 35); ulikuwa hazina iliyositirika na lulu bora ambazo kwa ajili yake mtu auze vyote kwa furaha (1C 35; AP 15; 29; L3C 33). Hata kabla hajaongoka hakuwa na uchu wa mali kama baba yake, hata akaonywa naye kwa ubadhirifu wa fedha katika anasa; baadaye alidharau utajiri na kupenda kuwashirikisha mafukara mali zake, hata aliposhtakiwa na baba akamrudishia kila kitu na kujinyima haki ya kumrithi. Kisha kubaki uchi mbele ya wote siku hiyo (1C 15; LJS 9; LMj II,4), alipenda daima kuonekana na kutendewa kama fukara. Siku nyingine ikambidi tena apunguze mavazi yake ili alingane na maagizo ya Yesu kwa mitume wake (1C 22; LMj III,1). Katika jitihada zake alifurahi mno kukaribia kifo akiwa hana hata kanzu ya kwake isipokuwa moja aliyoazima pamoja na kaptura na kikofia cha gunia, na hatimaye akafa uchi kama Yesu msulubiwa (1C 117; 2C 12; 215; LMj XIV,4).

4.2.2. ALIVYOJENGA JAMAA YAKE JUU YA UFUKARA

Fransisko hakuwa mchoyo kuhusu vitu wala kuhusu utajiri wake wa Kiroho (LJS 23); kwa hiyo kisha kuona faida ya ufukara aliwafundisha kwa bidii wafuasi wake wafuate njia hiyohiyo kwa mchakamchaka (LJS 24-26; LMj XIV,5), akionya vikali waliovunja masharti ya ufukara wa Kiinjili. Aliyasisitiza katika kanuni (ER I; XIV), kwa namna ya pekee katika sura ya sita ya ile ya kudumu (LR VI,1-6). Pia katika wasia mfupi, ule mrefu na ule aliomuandikia mtakatifu Klara alihimiza ufukara akiangalisha usiachwe kwa shauri la yeyote (UltVol). Ilimbidi autetee hasa mbele ya wasiwasi wa viongozi wa Kanisa: kwa ajili hiyo alijaliwa njozi ya mwanamke fukara aliyemzalia mfalme watoto wengi wasioweza kunyimwa riziki (ChOdo; 2C 16-17). Vivyo hivyo aliwahakikishia Ndugu Wadogo kuwa ulimwengu utawasaidia mahitaji yao mradi wazidi kutoa mifano mizuri (2C 70). Waliotaka kujiunga na shirika alikuwa akiwadai wayakane malimwengu na kumtolea Mungu mali zao kabla hawajajitoa wenyewe (ER XVII,5-18; LR II,5-8; Adm IV; XI; XIV; XIX; Test 16-17; 2C 140; 194): alikuwa hampokei mtu asiyekwishawagawia maskini vitu vyote kabisa alivyoagiza Yesu (2C 67; 81). Baada ya hapo ndugu walitakiwa kuridhika na chakula na mavazi tu, bila mali ya binafsi wala ya shirika (AP 27), kama walivyofanya wale wa kwanza walioishi naye Rivotorto katika hali ngumu ajabu wasilalamike (1C 42; 44; L3C 55; BPr II,1-9). Zamani hizo ndipo pesa ilipoanza kuenea sana, kukusanywa kwa wingi na kuwa sifa ya mtu mwenye uwezo. Kumbe yeye aliichukia kabisa (1C 9; 14; L3C 9; 2C 65) na kuwakataza Ndugu Wadogo wasiwe nayo (ER VIII; LR IV). Katika

kuidharau alifikia hatua ya kuwashauri waikimbie kama vile Shetani mwenyewe (2C 68; LMj VII,5) au kutoijali kama mavi au mavumbi (AP 30; L3C 35; AC 27; 2C 65).

### 4.2.3. ALIVYOKATAZA KUMILIKI MAENEO NA MAKAZI

Fransisko alikataa haki ya kumiliki: Ndugu Wadogo waishi kama wageni (2C 59) wasishindane na mtu kuhusu mahali popote kwa kuwa hakika si pa kwao (ER VII,13-14). Ndiyo sababu kila mwaka alikuwa akiwalipa Wabenedikto kodi fulani kwa ajili ya kikanisa cha Porsyunkula, maana yake Kasehemu (OL VII). Kwa namna ya pekee alitaka hiyo nyumba mama iwe na dhiki mfululizo kwa walioishi pale na kwa wageni wao kusudi pawe kielelezo kwa shirika lote (AC 56; 2C 18; OL VII). Hata mkutano mkuu wa ndugu elfu tano hivi ulifanyika huko pasipo jengo: wote walilala ardhini chini ya vibanda vya nyasi (AC 18). Alitaka ukubwa wa nyumba, kanisa na eneo la ndugu usipite kiasi kinachotakiwa na ufukara: kwa ajili hiyo alikataza ndugu wasikae wengi pamoja (AC 58), ila waishi katika nyumba duni au vibanda (Test 24; 2C 56; LMj VII,2), wakikumbuka kuwa Mwana wa Mungu hakuwa na mahali pa kulaza kichwa chake (1C 39; 52; AP 41; L3C 38; 59-60). Mwishoni wigo uwe wa miti, lakini si wa kuta (BPr IV,1-4). Mwenyewe alipendelea kutembelea na kuishi kidogo mahali fukara kuliko pengine, akitumia chumba cha kifukara zaidi, tena asisikie wanakiita "cha ndugu Fransisko", la sivyo atakihama (AC 57; 2C 59). Vilevile akisikia nyumba fulani inaitwa "ya ndugu" alikuwa akikataa kuingia, kama si kufukuza ndugu wote, wakiwa pamoja na wagonjwa (2C 58), au kuanza kuibomoa kabisa (AC 56; 2C 57).

### 4.2.4. ALIVYOHIMIZA KUBANA MATUMIZI YOTE

Fransisko alitaka kuumwa na ufukara, yaani kuonja shida za mafukara kama alivyofanya Yesu: ndiyo maana alibana sana matumizi, asije akachukua sehemu kubwa ya vitu na kuwakosea haki mafukara wengine (1C 41). Alikataza vifaa vya mezani na vya nyumbani visiwe vingi wala vya kilimwengu, kusudi kila kitu kitangaze hali ya kuwa wasafiri tu (1C 51; AC 25; 2C 60; 62), mafukara wakifika utawani wajisikie nyumbani, na watu wengine wajengeke. Sikukuu fulani alikataa kuketi mezani na wenzake kwa kuwa waliipamba mno, akala chini (AC 74; 2C 61); kumbe alifurahi akiona hakuna kilichoandaliwa na binadamu, isipokuwa zawadi za Mungu tu. Kuhusu vitabu, ambavyo zamani vilikuwa na thamani kubwa, alitaka viwe vichache na kutumiwa na wote bila ubinafsi (ER III,7-9; WBC V). Hakupenda kusahau kitabu cha Injili na ufukara wake kwa ajili ya hivyo vingine, tena alionya wenye elimu waache utajiri huo pia, wasije wakafundisha wengine bila kutekeleza wenyewe (Adm VII; 2C 185; 194; WBC IX). Alitaka ufukara mkuu ung'ae hasa katika mavazi; hivyo alikataa kanzu ya pili na vitu vingine, isipokuwa kamba na kaptura. Kanzu yenyewe ilikuwa ya kifukara sana, si ya kitambaa kipya, bali ya virakaviraka na yenye kukwaruza mwili wake. Alidai ufukara huohuo uwe na wafuasi wake, akiwakataza wasiwe na kanzu zaidi ya mbili wala laini (ER II,13-14; LR II,14-15; Test 16-17; 1C 39; AC 28-30; 2C 69; BPr IV,5-10). Alisisitiza sura ya nje iwe duni sana ili waeleweke mara kwamba ni wadogo; alitaka wasijali maneno ya watu (ER II,15), ila baraka itakayowafikia watakaozitia kanzu zao viraka ama kwa ukarabati ama kwa kupunguza baridi (LR II,16).

### 4.2.5. ALIVYOKULA JASHO LAKE

Fransisko hakupenda kunyonya kama watu wanaoishi bila kuwajibika, wakila jasho la wenzao, bali alitaka kustahili riziki kwa kufanya kazi kwa bidii (1C 39; 2C 161; LMj IV,3). Sababu nyingine za kufanya hivyo ilikuwa kukwepa uvivu, ulio adui wa roho na chanzo cha vishawishi vingi (AP 25; L3C 41; AC 107; 2C 160), kutumia vizuri muda aliojaliwa na Mungu (2C 97; 159; 161), na kujenga watu kwa kuwapa mfano mwema. Pamoja na hayo yanayomfaa kila mtu, alitaka Ndugu Wadogo wafanye hasa kazi za mikono chini ya wengine (ER VII,1-2; AC 56), bila kudai malipo (LR V,3-4; Test 20-22), tena bila kuzimisha roho ya sala (LR V,1-2). Kwa hiyo alitaka mafundi wawe na vifaa vyao ili kuendelea na kazi zao (ER VII,3-9), na wengine wote wajifunze kazi fulani (Test). Kwa umuhimu wake kazi ya mikono haitakiwi kuachwa na yeyote, hata kama ni mhubiri, mtu asije akafanana na nzi au nyuki dume asiyefanya kitu lakini anakula kabla ya wenzake (AC 48; 97; 103; 2C 75; 161; LMj V,6).

## 4.3. KUTII KWA UPENDO

Fransisko alianzisha jamaa ambamo utiifu wa kitawa utimizwe tofauti na mashirika mengine, yaani kwa msingi wa udugu unaofanya hata mwenye madaraka asiitwe baba wala mkubwa. Pamoja na hayo, utiifu wa Ndugu Wadogo ni imara kabisa (ER V,14-17; LR VIII,1; Test 27-30).

### 4.3.1. FRANSISKO NA UTIIFU

Fransisko anasifiwa kama mtu huru kweli; lakini alifikia uhuru huo kwa kunyosha utashi wake (3C 116). Ndiyo lengo la utiifu ambao ni kilele cha ufukara maana kwa kutii tunaacha si vitu tu, bali nafsi yetu yote mikononi mwa Mungu hasa kupitia viongozi (Adm III; 2C 140). Tukitii tunashinda maelekeo ya kibinadamu tu, tunaishi kwa amani na, jambo muhimu zaidi, tunatimiza matakwa ya Mungu yanayoweza kujitokeza hata kwa njia ya wanyama na matukio (SalV 14). Fransisko alifundisha tuwe tayari kutii si tu baada ya kuagizwa, bali tujitahidi kuhisi kiongozi anataka nini hata kabla hajasema (1C 45). Pia alitofautisha ngazi tatu za utiifu: ruhusa tunazopewa kwa kuziomba; maagizo ambayo ni bora kuliko ruhusa kwa sababu tunapewa bila kuyaomba; mwisho kuomba kwa wito wa Mungu tuende kueneza Injili kwa Waislamu na wengine wasio Wakristo: ombi hilo halitokani na ubinadamu wetu, nalo ni bora kabisa (ER XVI,3; LR XII,1; 2C 152; OL VI). Kadiri ya Fransisko, ndugu anapotenda mema akijua haendi kinyume na kiongozi wake, basi yuko chini ya utiifu vilevile. Tunatakiwa kujitahidi tutii matakwa ya Mungu ambayo kuyatambua ni kazi ya dhamiri: hatuwezi kumtii yeyote kinyume cha dhamiri au cha kanuni tuliyoitiwa (2Ltf 40-41; ER IV,3; V,2; LR X,1-3; OL III). Hivyo utiifu si kisingizio cha kutochukua jukumu la matendo yetu. Tena kati ya Ndugu Wadogo, wale wa chini wamepewa kazi ya kuchunguza matendo ya viongozi wao hata kuwalaumu, kuwashtaki na kuwaondoa madarakani kwa jina la Bwana (ER V; LR VIII; OL II). Pamoja na hayo, Fransisko alisikitika kuona ni vigumu kupata duniani kote mtawa mtiifu kweli ambaye kama maiti anaweza kutendewa lolote bila kubisha wala kudai kitu kingine, tena akiheshimiwa na kupewa cheo hajivuni (2C 152; LMj VI,4).

#### 4.3.2. MAMLAKA NI HUDUMA

Bwana Yesu alisisitiza neno hilo, na mfuasi wake Fransisko alilipokea kwa mikono miwili hata katika majina aliyotumia kwa wahudumu wa shirika lake: watumishi, watunzaji na walinzi; alikataa wasiitwe wakuu, wala wa kwanza wala baba (ER VI,3-4), bali waitwe kwa majina hayo ya Agano Jipya (ER IV,2-6; V,3-7; LR VIII; Test 27-33). Si suala la majina tu, bali alitaka watumikie kweli kwa unyenyekevu na upendo (2Ltf 42; Adm XXIV). Kwa sababu hiyo mhudumu awatembelee ndugu zake, awakosoe kwa upendo na kuwatendea kwa huruma (LR IV), hasa wakiwa na madhambi makubwa, akiepa hasira na fadhaiko, akubali wamtende kama mtumwa, awahimize kuomba msamaha, na atangaze atawapokea vizuri hata kama wamerudiarudia makosa (2Ltf 43-44; LtMin). Atende kama mzazi si kama dikteta (ER VI; LR X), na kutoa amri kwa utiifu mtakatifu katika nafasi za pekee tu. Fransisko alipochora taswira ya mhudumu bora (2C 185-187) alisisitiza sifa zifuatazo: awe na maisha magumu, asiwe mbaguzi, apende sala, unyofu na ufukara, awe mvumilivu kwa wote, tayari kufariji wenye huzuni na kujikatalia haki zake, mpole kwa wakosefu, mkali kwa wasengenyaji, atambue huduma kuwa mzigo kuliko cheo, asilegeze kamba katika jumuia, awe na adabu kwa watu wake, asitafute mashangilio bali wokovu wao, asitamani cheo bali akiogope (Adm IV; XIX; 1C 104). Katika hayo yote Fransisko alikuwa kielelezo (1C 41; 2C 180), akiwaombea sana ndugu aliokabidhiwa (2C 174), na kuwashughulikia wapate wokovu akiamini hatapokewa mbinguni bila wao (ER IV; V). Basi, wasije wakakosa mbingu pia baada ya kujinyima dunia, aliwahudumia akitumia upole wa kimama au adhabu kadiri ya mahitaji ya kila mtu (1C 51; AP 39; 2C 154; 177; LMj VI,11).

#### 4.3.3. ADILI LA UTIIFU

Unyenyekevu wa wahudumu hauondoi wajibu wa kutii walionao ndugu walio chini yao. Kwa Ndugu Wadogo kuweka ahadi ni hasa kupokewa katika utiifu kwa Papa na kwa mtumishi mkuu wa shirika (ER II,9-10; LR I,2-3; II,11-12; AP 36), hivyo asiyetii hastahili kuwa mtawa, afadhali arudie unovisi. Fransisko alisimulia alivyoona shingoni pa ndugu mkaidi yupo Shetani akimtawala anavyotaka (2C 34; LMj XI,11). Kwake mtawa nje ya utiifu yuko chini ya laana: amesahau alivyokana matakwa yake kwa upendo wa Mungu. Basi, amtii mhudumu wake hata akiyaona mengine kuwa bora zaidi. Amtolee Mungu sadaka hiyo mara anapoagizwa, bila kuchelewa wala kujisingizia kuwa agizo haliwezekani (2C 51). Mtawa atafaulu kutii hivyo hasa akizingatia kwamba mhudumu si binadamu duni bali anamwakilisha Kristo (2C 186), na kwamba Mungu anapendezwa hasa tunapomtii mtu asiye na sifa kuu (2C 151; LMj VI,4). Pia azingatie mzigo unaobebwa na wahudumu hata awapende na kuwaheshimu na kuwashughulikia katika mahitaji yao. Fransisko mwenyewe, akijua faida ya utiifu, alipenda kujiweka chini ya mwingine tangu mwanzo wa shirika hadi siku ya kufa, akijichagulia mlinzi au makamu ambaye alimuahidia utiifu kama mfungwa aliye mikononi mwake (Test 27-30; AP 31; 37; L3C 46; 57; AC 11; 2C 143; 151). Aliweza kukiri kuwa alijaliwa neema ya kumtii mlinzi hata kama angekuwa ameingia unovisi saa ileile. Kutokana na mifano yake bora ndugu wa kwanza walikuwa wakijitahidi kutambua hata mawazo yake ili kutii kabla ya kuagizwa (1C 39; AP 26; L3C 42). Hawakuweka chochote juu kuliko maagizo, na walipoachiwa kuamua wenyewe la kufanya walikuwa wakishangaa na kushindwa kuchagua (ChJG 18; 47).

# 5. ALIVYOSHINDA

Kisha kufurahia maadili ya Fransisko hata kutamani tuwe nayo, tuone kwa ndani zaidi alivyofikia utakatifu huo (Off 9:I-III). Ilimbidi ajitawale kikamilifu ili mwili uwe chini ya roho, na nafsi yake yote chini ya Roho Mtakatifu. Tena avumilie yote yaliyoruhusiwa na Mungu yatokee katika maisha yake.

## 5.1. ALIVYOJITAWALA

Juhudi za Fransisko kwa ajili ya utakatifu zilikuwa kubwa ajabu. Ingawa si rahisi kuziiga, ni vema kuzizingatia ili kupata changamoto na maelekezo.

#### 5.1.1. MALIPIZI YAKE

Kwa nini mtu huyo aliyetambua wema wa Mungu katika viumbe vyote aliutesa mwili wake (1C 53; L3C 20; 2C 12; 21; LMj II,4; V,6)? Maandishi yake yanasisitiza kwamba ni lazima wote wafanye hivyo ili waelekee unyenyekevu, subira, unyofu, amani ya roho, uchaji wa Mungu, hekima na upendo wa Kimungu (ER XVII,14-16). Alichota mafundisho hayo katika utajiri wa Kiroho wa maisha yake, ambamo alitekeleza maneno ya mtume Paulo kwamba tusulubishe mwili pamoja na vilema vyake na tamaa zake (LMj V,1). Akitamani kubeba msalaba wa Kristo si moyoni tu, bali mwilini pia (2C 210; LMj I,6), badala ya kulala kwa kawaida alikuwa akipata usingizi ameketi tu; kwa vyovyote hakukubali kutumia magodoro na mablanketi ila jiwe au ukuni kama mto, akiweka kanzu tu kati yake na ardhi (LMj V,1). Kwa kuwa binadamu anatafuta sana cha kula na cha kunywa, Fransisko aliona umuhimu wa kujishinda kikamilifu upande huo (L3C 14): kwa shida tu alikuwa akituliza kiu yake na kukubali vyakula vilivyopikwa; pengine aliviongezea majivu au maji mengi (1C 51; L3C 15; LMj V,1). Mwanzo wa ushindi huo ulipatikana kwa kula vile alivyoviombaomba akivikusanya katika bakuli moja. Pia alizoea kufunga chakula karibu mwaka mzima, akiyaongezea mafungo ya kanuni (ER III; LR III) mengine ya hiari kwa heshima ya Bikira Maria, malaika na watakatifu (2C 197; LMj IX,2-3). Alisema kuwa roho ikipoa, tamaa nyingine zinakuja kuwaka: mtu anaanza kuona kitu fulani ni cha lazima, kumbe sio (AC 28-30; 2C 69). Kinyume chake mtu akiwa na hitaji fulani, na kuvumilia bila kujipatia, ndipo anapostahili na kutuzwa. Katika njia hiyo aliweza kukiri mwili wake uliacha kupinga tamaa za roho tangu aongoke hadi kifoni. Ushindi huo ni wa ajabu hasa ukizingatia alivyokuwa dhaifu kiumbile na alivyozoea anasa (L3C 22; LMj II,7): waliomfahamu kwanza walimuonea huruma, lakini yeye hakuuonea huruma mwili wake, bali kila siku alikuwa akiona namna mpya za kuutesa (AC 50; 2C 129). Karibu na kufa tu alikiri ametesa mno mwili wake hata akauomba msamaha (2C 210-211). Alifaulu hivyo kutokana na neema na bidii alizokuwa nazo toka mwanzo alipokwenda kuwatumikia wakoma hata akala nao sahani moja: kwa

ushindi huo mkuu alilinganisha matakwa ya mwili na ya roho (L3C 11; 2C 9; LMj I,6) akamtolea Mungu vyote alivyonavyo (1C 97; LMj V,9).

### 5.1.2. ALIVYOTAWALA MOYO NA HISI

Moyo unatokwa na maovu yote (2Ltf 7), hata inawezekana kusema hakuna adui mkubwa zaidi (2C 134): unahitaji daima kufanyiwa utambuzi kwa kuwa unaweza kupotosha hata matendo mema. Pamoja na kutawala hisi zake zote, kuanzia macho (1C 43), Fransisko alikuwa akizuia ulimi usiseme maneno ya bure ambayo kwa mtawa asiyefaa ndiyo furaha kuu (Adm XXI). Kumbe mtawa mwema anaonja heri katika maneno ya Mungu, asipende kupoteza faida hiyo ya sala kwa kuongea bure (AC 108; RH). Zaidi ya kutoa mawaidha hayo, Fransisko aliagiza adhabu kwa watakaokwenda kinyume.

### 5.1.3. MALIPIZI NA BUSARA

Fransisko alikuwa mkali sana kwake, lakini aliwahurumia wenzake na kuwafundisha wasipite kiasi katika malipizi kwa kufuata kiburi chao au shauri la Shetani (Adm XXVII; L3C 59; AC 50; 2C 21; LMj V,7). Alifananisha mwili na punda ambaye, asipopewa chakula cha kutosha, ana haki ya kugoma, lakini akigoma kisha kushiba ahimizwe kwa mapigo; hivyo mwili upatiwe mahitaji yake (CtExt; 2C 22), halafu uwajibishwe katika sala na kazi (AC 120; 2C 129). Katika hali wazi ya shida aliruhusu ndugu wasitimize sheria fulani (ER IX; XV; LR II; III), akawashauri viongozi pia wajipatie mahitaji ya pekee bila kufichama, kusudi wengine wasione aibu kufanya vilevile (2C 68).

## 5.2. ALIVYOVUMILIA MAJARIBU YOTE

Fransisko alifanya malipizi makali ili ajishinde, hata hivyo ushindi mkubwa zaidi ulikuwa kuvumilia matatizo ambayo hayakutarajiwa lakini Mungu aliyaruhusu ili yamkamilishe. Hasa ilimbidi adhulumiwe kwanza na ndugu zake wa ukoo, halafu na ndugu wa shirika lake; pia Shetani alimjaribu kwa namna nyingi za kutisha.

### 5.2.1. NDUGU WA UKOO WALIVYOMDHULUMU

Ilimbidi Fransisko atengane kikamilifu na yote ili aambatane na Yesu msulubiwa. Basi, kwa maongozi ya Mungu alianza kudhulumiwa na watu wa ukoo wake, hasa baba (1C 10; 12-13; LJS 7-8; AP 8; L3C 18-20; 23; 2C 12; LMj II,2-3), na wa mji wake (1C 11; AP 9; L3C 17), akakubali kutupwa nao kwa ajili ya Kristo: alifungwa, alitukanwa, alilaaniwa, alipigwa, alichekwa, alirushiwa matope na mawe, alishtakiwa mbele ya serikali na ya askofu, akabaki peke yake, wa pili Mungu, lakini hakurudi nyuma (LCh 3; AP 16; 20; 23; L3C 34; 37-38; 40; 62; LMj IV,7).

### 5.2.2. NDUGU WADOGO WALIVYOMPINGA

Upinzani mbaya na wa muda mrefu zaidi ulimpata Fransisko kutoka kwa wafuasi wake aliowapenda mno (1C 28). Huo ulihusu mtindo wa maisha alioangaziwa na Mungu katika Injili na kwa njia ya sala (AC 16; WSF 2; WBC I,1-4). Hasa alipingwa na viongozi wa shirika na ndugu wenye elimu waliotaka Ndugu Wadogo wafuate taratibu za watawa wengine (OL IV; V); halafu iwepo hakika fulani ya kupata riziki kwa umati wa wanashirika (AC 16; WSF 2; WBC I,6-15). Ndugu hao walijitahidi kuvuta upande wao viongozi wa Kanisa, hasa kardinali Hugolino wa Ostia, msimamizi wa shirika (Off 1:III; AC 18; WSF 4). Fransisko alisikitika sana (AC 112; 2C 158) kuona wanavyotaka kupotosha kazi ya Mungu inayotarajiwa kuokoa watu wengi (OL I; WBC X). Akiogopa waamini watakwazwa na mabishano hayo, aliacha kuandika wazi katika kanuni baadhi ya mambo, akayaandikisha katika barua zake na katika wasia; hata hivyo aliendelea kutetea ukamilifu wa Injili akikubali kuonekana mpumbavu na kichaa, si kusogea mbali na njia ya unyofu na ufukara (AC 106). Hatua ya kusikitisha sana katika historia ya shirika ni ile aliyoichukua alipong'atuka ingawa angekuwa tayari kuendelea na uongozi akiwa mgonjwa kitandani (2C 143). Lakini alipenda kuongoza kwa mahubiri na mifano yake kuliko kwa ukali na adhabu; hivyo alipoona wengi hawataki kufuata nyayo zake, tena wanapuuzia mafundisho yake (AC 21; WSF 5), aliamua kuacha uongozi na kutumaini Bwana atawarudisha kwa namna moja au nyingine.

### 5.2.3. SHETANI ALIVYOMSHAWISHI NA KUMTESA

Adui wa Mungu anawajaribu daima watu wote, lakini kwa namna ya pekee watakatifu (2C 120). Fransisko pia alishawishiwa na kuteswa sana na Shetani katika jitihada za kumzuia asichangie urekebisho wa Kanisa (2C 116; LMj V,4). Lakini bure, kwa sababu Fransisko alimshinda daima kwa neema ya Mungu (AC 63; 2C 108; 115; 122; LMj VI,9; X,3; X,6). Baadhi ya mbinu alizozitumia Shetani toka mwanzo ni kumtisha kuwa atamharibu awe na sura ya mwanamke fulani mwenye kibyongo (L3C 12; 2C 9), kumpiga usiku kucha (AC 117; 2C 119; LMj VI,10), kusababisha kelele na maporomoko ya kutisha (1C 72), kuzidisha panya wapite juu yake usiku na mchana wakati wa ugonjwa (AC 83), kumlevya kwa kufichama ndani ya mto alioutumia kulaza kichwa chake (AC 119; 2C 64), kumsukuma atumbukie gengeni, mbali na vishawishi vingine vya kawaida kama vile vya uzinifu. Ugumu wa mashindano unaeleweka tukizingatia kuwa Fransisko, askari shujaa, alifikia hatua ya kusema, "Ndugu wangejua dhiki na tabu wanazonipa mashetani ni nyingi tena kubwa namna gani, wote wangenionea huruma na imani" (AC 118; 2C 213).

### 5.2.4. MAFUNDISHO YAKE KUHUSU MAJARIBU

Kwa kuwa alijaribiwa hivyo, mtakatifu wetu anafaa sana kutoa mashauri ya kufuatwa vitani (1C 117): la msingi ni kuwa tusisahau Neno la Mungu na utumishi wake kwa kuvutiwa na jambo au shughuli yoyote (ER XXII). La pili ni kuweka uchaji wa Mungu kama mlinzi wa roho yetu (Adm XXVII). La tatu ni kudumisha moyo wa ibada na furaha kwa njia ya sala na matendo mema (AC 120), bila kumuachia Shetani hata nafasi ndogo, la sivyo atageuza haraka unywele uwe boriti kwa kuzidisha dhambi. La nne ni kufukuza hofu yoyote kwa kutegemea msaada wa Mkombozi. La tano ni kuutesa mwili (ER XXII; LMj V,2) ikiwa kishawishi kinahusu uzinifu, kama alivyofanya yeye. La sita ni kuzingatia majaribu ni ishara ya mtu kumpenda Mungu, na yale makali zaidi yanathibitisha kuwa si

dhaifu (2C 118). Kwa imani alitambua na kufundisha kwamba, kuadhibiwa na Mungu kwa matatizo mbalimbali yanayotupata duniani ni alama ya upendo wake, kwa kuwa hivyo anakosoa asije akaadhibu baada ya kifo. Basi ni lazima tupokee mateso yote (TPJ) kwa uvumilivu, tena kwa furaha, na hasa kwa upendo wa Yesu aliyeyavumilia kwa ajili yetu: kufanya hivyo ni kama kufia dini. Faida nyingine ni kwamba katika mapingamizi mtu anaona subira na unyenyekevu alionao kweli (Adm XIII), kwa kuwa katika hali ya kuridhisha ni rahisi kudanganyika kutokana na sala na mafungo; kumbe akipigwa au kunyang'anywa kitu au kuambiwa neno baya, anashindwa kujichukia na kupenda maadui. Maneno ya Fransisko kuhusu ufukara wa roho na kuhusu kujitoa moja kwa moja yanatuhimiza kukubali mambo yoyote kama neema ya Mungu, tukitii mapenzi yake hata yawe mbele kuliko mipango yetu, ikiwa ni pamoja na ule wa kujitafutia ukamilifu kwa njia fulani (LtMin 1-8). Aliyoyafundisha yeye aliyatekeleza, hasa mbele ya upinzani alioukabili kwa ustahimilivu na kwa kukimbilia sala.

5.2.5. ALIVYOPOKEA KWA FURAHA MARADHI NA MATESO MAKALI

Fransisko akiwa dhaifu kwa umbile, tena zaidi baada ya kwenda vitani na kufungwa (1C 3; L3C 6; LMj I,2), kutokana na ugumu wa maisha aliyojichagulia nyuma ya Yesu (AC 51; 1C 56; 97; 3C 34; LMj IX,6) aliugua muda mrefu maradhi mbalimbali (2Ltf; LtOrd; Test; 1C 105; AC 59; 96) hadi akafa kwa malaria (2C 214; 3C 37; LMj VI,2). Karibu viungo vyake vyote, hasa macho, maini na tumbo (2C 96; 105; 130; LMj V,11; X,6), vilikuwa na mateso makali kuliko ya kifodini chochote (1C 107). Mwili wake ulibaki mifupa na ngozi tu, lakini alipokea maradhi kama ishara ya wema wa Bwana asipotewe na utulivu na furaha (1C 98; LMj V,8). Alikuwa akiyaita "ndugu" na kujiombea azidishiwe mara mia ili kutimiza mapenzi ya Mungu (2C 212; LMj XIV,1-2): ni kwamba kwa kuzingatia yale ya Yesu na kwa kutamani kumuiga alikuwa hajali ya kwake mwenyewe (AC 77). Mbali ya maradhi, aliteswa vibaya na matibabu pia (1C 98; 101; LJS 65-66; AC 83; 86; 2C 166; 215; 3C 14; LMj V,8-9). Pamoja na hayo, Mungu alimuongezea kwa namna ya ajabu mateso ya madonda ya Mwanae msalabani ambayo yalimfariji sana Kiroho, lakini yalifanya mwili wake usiwe na raha tena, ukitokwa na damu hata kutiririka (1C 94; ChRog 10-12; LCh 11; Off 21; LJS 61-63; WS; L3C 17; BO; LMj XIII,3). Hata hivyo alitamani kuanza upya maisha ya toba kama kwamba hajafanya sana (LJS 67) hakukubali kwa urahisi kupunguza ugumu wa maisha yake wala kutibiwa wala kula vitu vya kumfaa zaidi katika ugonjwa (AC 80-82). Vilevile alitaka wafuasi wake wagonjwa wapokee mapenzi ya Mungu kwa shukrani bila kuwalalamikia Mungu na wenzao (CtC 10-11): aliona kufanya kinyume ni kuonyesha upendo mkubwa kwa mwili kuliko kwa roho (ER X,3-4). Mwenyewe aliyapokea kwa shangwe rohoni na kwa kukimbilia muziki (2C 212-213) hata alipozidiwa alitunga wimbo wa kumsifu Mungu kwa viumbe vyake (CtC 1-9, 14), akigeuza hivyo uchungu uwe utamu (AC 83).

5.2.6. ALIVYOKARIBISHA NDUGU KIFO

Siku za mwisho za maisha yake zilijaa nyimbo usiku na mchana, kiasi cha kushangaza wenye imani haba: ilimbidi awaeleze kwamba hayo yalitokana na umoja wake na Bwana, uliofanya kuishi au kufa kuwe mamoja kwake (AC 100). Ndiyo maana alipoambiwa kifo kimekaribia alikikaribisha kwa furaha kubwa (2C 217; LMj XIV,5) na kuongeza beti za kumsifu Mungu kwa ajili ya ndugu kifo (CtC 12-13; 1C 109; AC 7). Hivyo alifariki kwa kuimba (LCh 12; LJS 69; AC 99) huku amelala uchi ardhini (L3C 68; 2C 214; 216; 3C 5; LMj XIV,3) akiwa na umri wa miaka 44 tu. Miujiza aliyojaliwa kufanya akiwa hai (LCh 10; LJS 47-56) ilizidi kutokea alipoombwa kisha kufa kwake (LCh 13-16; Off 25) hata miaka miwili tu baadaye akatangazwa na Papa Gregori IX kuwa mtakatifu (LCh 17; Off 1:II; LJS 73-76).

## VYANZO VILIVYOTUMIKA

Kitini hiki kimefupisha habari zinazopatikana katika vyanzo vya karne XIII: kwanza maandishi ya Fransisko mwenyewe, halafu yale ya wengine, wawe wafuasi wake au sio. Si ajabu kwamba habari nyingine zinarudiwarudiwa na vyanzo hivyo. Kadiri iwezekanavyo, madondoo yamepangwa katika mabano kadiri ya tarehe ya vyanzo hivyo kuandikwa.

Maandishi yote ya Fransisko na ya Klara na machache mengine (ScEx; L3C) yametafsiriwa na Ndugu Wadogo Wakapuchini kwa Kiswahili. Kwa vyanzo vingine ni lazima kutumia lugha asili au tafsiri mojawapo. Kwa Kiingereza matoleo ya kitaalamu zaidi ni:

- Francis of Assisi: Early Documents - ed. New City Press (vitabu 3)
- Clare of Assisi: Early Documents - ed. Franciscan Institute Publications

VIFUPISHO VYA MAANDISHI YA MT. FRANSISKO

| | |
|---|---|
| 1LtCl | Barua I kwa Wakleri |
| 1LtCus | Barua I kwa Watunzaji |
| 1Ltf | Barua I kwa Waamini |
| 2LtCl | Barua II kwa Wakleri |
| 2LtCus | Barua II kwa Watunzaji |
| 2Ltf | Barua II kwa Waamini |
| Adm | Mawaidha |
| BlL | Baraka kwa Ndugu Leo |
| CtC | Wimbo wa Viumbe |
| CtExh | Wimbo wa Himizo |
| ER | Kanuni ya Muda |
| ExhP | Himizo la Kumsifu Mungu |
| FormViv | Mtindo wa Maisha kwa Mabibi Fukara |

| | |
|---|---|
| LR | Kanuni ya Kudumu |
| LtAnt | Barua kwa Mt. Antoni |
| LtL | Barua kwa Ndugu Leo |
| LtMin | Barua kwa Mtumishi |
| LtOrd | Barua kwa Shirika Lote |
| LtR | Barua kwa Watawala |
| OfP | Ofisyo ya Mateso |
| PrCr | Sala Mbele ya Msulubiwa |
| PrOF | Ufafanuzi wa Baba Yetu |
| PrsG | Masifu ya Mungu |
| PrsAH | Masifu Kabla ya Kila Kipindi |
| RH | Kanuni kwa Makao ya Upwekeni |
| SalBVM | Salamu kwa Bikira Maria |
| SalV | Salamu kwa Maadili |
| Test | Wasia |
| TPJ | Furaha Kamili |
| UltVol | Matakwa ya Mwisho kwa Mt. Klara |

## VIFUPISHO VYA MAANDISHI YA MT. KLARA

| | |
|---|---|
| 3LAg | Barua III ya Mt. Klara kwa Mt. Agnes wa Praha |
| BCl | Baraka ya Mt. Klara |
| RCl | Kanuni ya Mt. Klara |
| TestCl | Wasia wa Mt. Klara |

## VIFUPISHO VYA VYANZO VINGINE VYA KARNE XIII

| | |
|---|---|
| 1C | Maisha ya Mt. Fransisko yaliyoandikwa na Thoma wa Celano |
| 1LtJV | Barua I ya Yakobo wa Vitry |
| 2C | Kumbukumbu ya Hamu ya Roho iliyoandikwa na Thoma wa Celano |
| 3C | Kitabu cha Miujiza kilichoandikwa na Thoma wa Celano |
| 6LtJV | Barua VI ya Yakobo wa Vitry |
| AC | Mkusanyo wa Asizi |
| AP | Simulizi la Yohane wa Perugia |
| BC | Hati ya Papa Aleksanda IV ya Kumtangaza Klara Kuwa Mtakatifu |
| BO | Hati “Benigna Operatio” ya Papa Aleksanda IV |
| BPr | Kitabu cha Wasifu kilichoandikwa na Bernardo wa Besse |
| CD | Hati “Cum Dilecti” ya Papa Honori III |
| ChAlb | Mambo ya Nyakati yaliyoandikwa na Alberiko wa Trois-Fontaines |
| ChBer | Mambo ya Nyakati yaliyoandikwa na Bernardo Mwekahazina |
| ChBur | Mambo ya Nyakati yaliyoandikwa na Burchard wa Ursperg |
| ChErn | Mambo ya Nyakati yaliyoandikwa na Ernoul |
| ChJG | Mambo ya Nyakati yaliyoandikwa na Jordano wa Giano |
| ChLau | Mambo ya Nyakati ya Lauterberg |
| ChOdo | Mahubiri yaliyoandikwa na Odo wa Cheriton |
| ChRich | Mambo ya Nyakati yaliyoandikwa na Richer wa Sens |
| ChRog | Mambo ya Nyakati yaliyoandikwa na Roger wa Wendover |
| CS | Hati “Cum Secundum” ya Papa Honori III |
| ExSt | Mifano ya Stefano wa Bourbon |
| HOcc | Historia ya Magharibi iliyoandikwa na Yakobo wa Vitry |
| HSal | Historia Saloniana iliyoandikwa na Thoma wa Split |
| InsL | Maelezo ya Ndugu Leo |
| JL | Barua ya Pamoja ya Hubert of Romans na Yohane wa Parma |
| L3C | Ngano za Wenzi Watatu |
| LCh | Maisha ya Kusomwa katika Liturujia yaliyoandikwa na Thoma wa Celano |
| LCl | Maisha ya Mt. Klara |
| LivBr | Maisha ya Ndugu yaliyoandikwa na Gerard wa Frachet |
| LJS | Maisha ya Mt. Fransisko yaliyoandikwa na Juliani wa Speyer |
| LMj | Simulizi Refu la Mt. Bonaventura |
| Off | Matini ya Liturujia yaliyoandikwa na Juliani wa Speyer |
| OL | Simulizi la Zamani |
| PasSV | Mateso ya Mt. Verekondo |
| PD | Hati “Pro Dilectis” ya Papa Honori III |
| QA | Hati “Quoniam Abundavit” ya Papa Gregori IX |
| QP | Hati “Quia Populares” ya Papa Honori III |
| ScEx | Sacrum Commercium au (Agano Takatifu la) Mt. Fransisko na Bibi Ufukara |
| VD | Hati “Vineae Domini” ya Papa Honori III |
| WBC | Maneno ya Nd. Konrado |
| WS | Walioshuhudia Madonda |
| WSF | Maneno ya Mt. Fransisko |